SportPesa
TZS. 450,150,500
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Wachungaji** 17 wafukuzwa kazi mgogoro KKKT

UKURASA 4


Darasa la wanawake wauza dagaa DRC
Corona ilivyowaletea neema wanakijiji mbegu za mahindi
BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
ESTHER LEMA:
Kutoka kuuza lita moja ya asali hadi kusafirisha tani kadhaa nje ya mipaka

UKURASA 11

Nipashe
Ijumaa Agosti 27, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580685
www.ippmedia.com
MWANGA WA JA
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# MAPYA ZAIDI MAUAJI YA DAR

**ALIYEFYATUA RISASI ADAIWA ALIWAHI KUJIRUSHA GHOROFANI, ANA ULEMAVU WA MGUU. MAJIRANI, DIWANI WALONGA...**

*Endelea ukurasa 2*





UKURASA 2

## Kamati ya Bunge yaagiza Mbunge Silaa akamatwe

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### SABAYA KIZIMBANI KESI UHUJUMU UCHUMI

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wenzake saba leo wanatarajiwa kupandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha kusomewa maelezo ya awali ya kesi inayowakabili mahakamani huko.

UKURASA WA 4

### SAMIA APOKEA HATI ZA UTAMBULISHO MABALOZI WATANO

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alipokea hati za utambulisho wa mabalozi watano walioteuliwa kuziwakilisha nchi zao nchini.

UKURASA WA 4

### ZITTO KABWE AAHIDI MABORESHO TCD

MWENYEKITI wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Zitto Kabwe, ameahidi kuhakikisha kwa kipindi cha miezi sita mazingira ya kufanyia kazi ya watumishi na wadau wa kituo hicho yanaboreshwa na kukirudisha kwenye hadhi yake.

## Jela mwaka mmoja kwa kumtukana mama mzazi

UKURASA 3



Zarina Sadiki (kulia), akiingia kwenye chumba cha polisi katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam jana, baada ya mahakama hiyo, kumtia hatiani na kumhukumu kwenda jela mwaka mmoja kwa kosa la kutumia lugha ya kuudhi na kumtukana mama yake mzazi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**MICHEZO** JEMBE ULAYA AKUNWA WAKONGO KIKOSI YANGA UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mapya zaidi mauaji Dar

**Na Waandishi Wetu**

TUKIO la mauaji ya askari mkoani Dar es Salaam limeendelea kuibua utata, huku majirani na uongozi wa eneo alikokuwa anaishi anayedaiwa kuyatekeleza, wakisimulia maisha ya kijana huyo.

Baadhi ya majirani, akiwamo Venance Kalunga, katika mazungumzo na Nipashe jana, alidai kuwa juzi asubuhi walikuwa na kijana huyo maeneo ya nyumbani huko Mtaa wa Mataka na Senegal, Kata ya Upanga jijini.

Alidai kuwa wakiwa kwenye maeneo hayo, walikunywa kahawa na katika mazungumzo yao, kijana huyo alikuwa na malalamiko aliyotoa kwamba alikuwa na msongo wa mawazo.

Kalunga alisema amemfahamu kijana huyo aliyemtaja kwa jina la Hamza tangu mwaka 1991, yaani miaka 20 iliyopita.

“Alikuwa mtu mwadilifu na utukutu alikuwa nao lakini haukuwa wa kutumia silaha wala wizi, sikuwahi kujua kama anamiliki silaha, wala sijajua ameitoa wapi. Ninachofahamu Hamza alikuwa anafanya kazi mgodini.

“Inawezekana alipata silaha baada ya kupata mali, mara ya mwisho kuonana naye ilikuwa jana (juzi) asubuhi, alisema ana msongo wa mawazo, wakati huo alikuwa anakunywa kahawa, kuna wazee huwa anakaa nao asubuhi, alikuwa anasema ‘leo nina msongo wa mawazo isivyo kawaida’,” alidai.

Kalunga alidai kuwa baada ya kunywa kahawa majira saa mbili asubuhi wakati watu wanakwenda kazini, alirudi kwao na baadae akaona kwenye mitandao ya kijamii tukio hilo alilolifanya.

“Sijawahi kuiona silaha yake, mara nyingi huwa katika migodi yake, miezi kadhaa iliyopita alirudi kutoka Misri. Alivyorudi aliingia mgodini, akauendesha, akafanikiwa akanunua gari na pikipiki, akipata fedha akija anatuambia jamani kunyweni kahawa,” alisema.

Alidai kuwa hata juzi wakati wanakunywa kahawa, waliamini amefanikiwa kama kawaida yake, lakini tukio lilivyotokea walishangaa.

“Tulishangaa, maadili hayo ameyatoa wapi? Na kwa nini anafanya hivyo? Wito wangu kwa vijana hata kama unakwazwa kwenye uendeshaji magari, labda trafiki amekukwaza, usitumie hasira au silaha kuumiza.

“Kwa Jeshi la Polisi wawe makini, uhifadhi na umiliki silaha wakati wakiwa lindo, tumeona jana (juzi) silaha tatu zimetumika pale, silaha ndogo na mbili zilizotoka kwenye vibanda vya polisi,” alisema na kulishauri jeshi hilo lisimilikishe silaha watu ambao wana chembechembe za kuwa na matatizo ya akili.

“Hamza alikuwa na aina ya utukutu uliozidi ila ilikuwa kipindi cha nyuma kidogo, kuna kipindi aliruka ghorofani pale kwao akavunjika mguu. Kwa hiyo pale ana ulemavu wa mguu,” alidai.

Alidai mama yake alikuwa anajua ni mtukutu na hicho ndicho kinaaminika kuwa sababu ya kupelekwa Misri kufanyiwa dua.

Diwani wa Upanga Magharibi, Adnan Kondo, aliiambia Nipashe jana kuwa walipokea kwa mshtuko taarifa za tukio hilo, akibainisha kuwa kijana huyo alikuwa anaishi na mama yake na ni mkazi wa muda mrefu wa eneo hilo.

“Kwa tabia hakuwa na tabia nzuri, lakini hatukumjua sana kama tayari alishawahi kumpiga mtu au la, sijasikia kijana ambaye anamsifu kwamba alikuwa na tabia nzuri, sijasikia jirani ambaye anasema alikuwa na tabia nzuri, hili sijapata kusikia,” alisema.

Kiongozi huyo alitoa wito kwa wananchi wa eneo hilo kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi endapo watatakiwa kutoa taarifa zozote kuhusu kijana huyo, akikiri kuwa tayari viongozi wa eneo hilo, akiwamo yeye, wamehojiwa na jeshi hilo kuhusiana na tukio hilo.

HALI ZA MAJERUHI

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Umma Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Aminiel Aligaesha, alisema jana kuwa walipokea majeruhi watano juzi kuanzia majira ya saa saba mchana wakiwa na majeraha makubwa na wengine madogo.

Aligaesha alisema wanne kati yao ni askari wa Jeshi la Polisi na mmoja ni mlinzi wa kampuni binafsi ya SGA.

“Mara tu baada ya kupokewa, askari wawili mwenye umri wa miaka 41 na mwingine miaka 49, walikuwa na majeraha makubwa katika sehemu mbalimbali za mwili na ya viungo vya ndani, hivyo kufanyiwa upasuaji wa haraka ambapo upasuaji ulienda vizuri,” alisema.

Alisema askari wa tatu mwenye umri wa miaka 35, alipata majeraha makubwa na madogo katika maeneo ya mikono na mgongoni. Alipewa huduma stahiki na kufungwa vidonda.

Alisema mwingine mwenye miaka 46 alitibiwa na kuruhusiwa kwenda nyumbani kwa kuwa alikuwa na majeraha madogo.

“Mlinzi wa SGA miaka 42, alikuwa na majeraha ambayo hayakuhitaji upasuaji. Hata hivyo, alilazwa wodini jana (juzi) na ameruhusiwa leo (jana) kwenda nyumbani kuendelea na matibabu akiwa nyumbani,” alisema.

Aligaesha alisema wamebakiwa na majeruhi watatu ambao wanaendelea kupata matibabu na hali zao zinaendelea kuimarika.

Pia alisema walipokea mwili wa mtu mmoja kutoka kwenye tukio hilo ambaye alikuwa ni mlinzi wa SGA na umehifadhiwa chumba cha kuhifadhi maiti.

Katika tukio hilo ambalo kiini chake bado kiko gizani, watu watano walifariki dunia akiwamo kijana huyo, askari watatu wa Jeshi la Polisi na mmoja wa Kampuni ya SGA.

***Imeandaliwa na Romana Mallya na Kalebo Mussa (TUDARCo)***

# Kamati ya Bunge yaagiza Mbunge Silaa akamatwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imemwomba Spika kuidhinisha Mbunge wa Ukonga (CCM), Jerry Silaa, akamatwe kwa kukaidi kufika kuhojiwa kwa mara ya pili na kamati hiyo.

Kutokana na mbunge huyo kutofika mbele ya kamati hiyo jana, imemwomba Spika Ndugai kutoa kibali cha kukamatwa na kumfikisha mbele ya kamati leo saa nne asubuhi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Emmanuel Mwakasaka, alisema jana kuwa shahidi huyo alipaswa kufika mbele ya kamati hiyo jana saa tano asubuhi lakini hakufika na hakutoa taarifa yoyote ya kutofanya hivyo.

“Leo (jana) tulikuwa tunaendelea na shauri la Mheshimiwa Silaa ambaye hajafika mbele ya kamati hii na hatuna taarifa yoyote ya kwa nini hatofika kwenye kamati hii.

“Sasa sisi kwa mujibu wa kanuni na sheria ambazo ni za Haki, Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Spika yeye ndiye mleta shauri. Kwa hiyo, kwa kutumia sheria hizo nimeomba kibali kwa Spika ili akamatwe na kuletwa hapa kama sheria zetu zinavyoturuhusu,”alisema.



Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Emanuel Mwakasaka, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, baada ya kuahirisha kikao cha kamati hiyo kilichokaa kwa ajili ya kumhoji Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa ambaye hakuonekana na hivyo ameagiza kukamatwa na vyombo vya ulinzi na usalama ili kufikishwa mbele ya kamati hiyo, leo. Kulia ni Katibu wa Kamati hiyo, Maria Mdulugu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Mwakasaka alisema Spika akiridhia, shahidi huyo atapelekwa mbele ya kamati kwa mujibu wa sheria.

“Sisi tulimwita ili tuendelee na shauri lake maana juzi tulimwita na kwa kawaida anaendelea na kiapo chake kilekile, tumemsubiri kwa muda wa kutosha lakini hakuna taarifa yoyote,” alisema.

Alibainisha kuwa kwa mujibu wa sheria, kwa kuwa mbunge huyo hakupeleka taarifa, hati ya kukamatwa inapaswa kuandaliwa.

“Kwa hiyo sisi kama kamati tumemwomba Mheshimiwa Spika, tunasubiri kibali chake ili ikiwezekana kesho (leo) saa nne asubuhi aweze kuletwa hapa na vyombo vinavyohusika na mambo ya usalama.

“Kibali cha kukamatwa hutolewa hata mahakamani kwa yule aliyepewa jukumu la kumkamata huyo mtu muda wowote. Sasa anahifadhiwa wapi hadi kuletwa eneo la mahojiano hilo linakuwa chini ya watu wa usalama,” alisema.

Agosti 23, mwaka huu, mbunge huyo alifika mbele ya kamati hiyo kufuatia wito wa Spika kutokana na tuhuma mbalimbali zinazomkabili ikiwamo kusema uongo na kushusha hadhi na heshima ya Bunge.

Agosti 21, mwaka huu, Spika Ndugai aliagiza mbunge huyo kufika mbele ya kamati kwa mujibu wa kanuni ya 4(1)(a) na (b) ya nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni 2020 ambayo inaipa mamlaka kamati hiyo kuchunguza mambo yanayohusu maadili ya wabunge yanayopelekwa kwa Spika.

# Wajisaidia vichakani kwa ukosefu wa vyoo

**Na Happy Severine,** BARIADI

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Kidinda katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu, wanajisaidia vichakani kutokana na vyoo vilivyopo shuleni hapo kujaa.

Walitoa kilio hicho jana wakati wa kupokea kompyuta tano zilizotolewa na Mbunge wa Bariadi, Kundo Mathew, zilizotolewa shuleni hapo kwa ufadhili wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

Walisema kuwa wamekuwa wakijisaidia vichakani kwa kipindi kirefu kutokana na matundu yao yote ya vyoo ambayo ni manane kujaa.

"Siyo siri vyoo vyetu vimejaa vyote na kwa hali hiyo wanafunzi tunalazimika kujisaidia vichakani hali ambayo inahatarisha usalama wa afya zetu na uchafuzi wa mazingira yetu ambayo kwa sasa kila sehemu kumetapakaa harufu ya mkojo na vinyesi," alisema mmoja wa wanafunzi hao, Gila Masanja.

Alisema shule hiyo yenye wanafunzi 1,075, ina vyoo vyenye matundu manane tu ambayo yamejaa na yenyewe hali ambayo imewalazimu kupata huduma hiyo kwa shida, huku wengine wakijisitiri katika vichaka vilivyopo shuleni.

Mwanafunzi wa kidato cha nne, Charles Bahame, alisema kitendo cha wanafunzi kujisaidia ovyo hadi kwenye maeneo ya shule, kimesababisha baadhi yao kuumwa matumbo mara kwa mara, hali inayotishia usalama wa afya zao.

Mkuu wa Shule hiyo, Mhinga Malongeta, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na kumwomba mbunge kuwasaidia katika ujenzi wa vyoo hivyo.

"Kwa kweli wanafunzi wana changamoto kubwa na hasa hii ya ukosefu wa matundu ya kutosha ya choo na kusababisha wajisaidie kwa zamu na tena sehemu moja bila kujali jinsi yao," alisema.

"Upungufu ni mkubwa wa vyoo jamii na wazazi tayari tumewashirikisha kuchangia ujenzi, waliokuwa tayari kuchangia ni kwa hali na mali wachache na wengine wamejitolea ili kuhakikisha choo cha matundu nane kinajengwa" aliongeza.

# Jela mwaka mmoja kwa kumtukana mama mzazi

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Ilala imemtia hatiani na kumuhukumu kwenda jela mwaka mmoja Zarina Sadiki kwa kosa la kutumia lugha ya kuudhi na kumtukana mama yake mzazi.

Zarina alihukumiwa jana mbele ya Hakimu Mfawidhi, Martha Mpaze, baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mpaze alisema Zarina anadaiwa Novemba 29, 2019, maeneo ya Kariakoo, Uhuru na Nyamwezi, alimtukana mama yake, Rafika Sadiki.

Hakimu alisema mshtakiwa anadaiwa kumwambia mama yake chizi, malaya mkubwa, sio mama yake, baba yake hajakumwoa, mwanaharamu, mwizi mkubwa, atahakikisha amemuua kwa njia yoyote ile au atamwagia tindikali afie mbali, maneno ambayo yalisababisha uvunjifu wa amani.

Katika kesi hiyo, Upande wa Mashtaka ulikuwa na mashahidi wanne, akiwamo mama mzazi na mshtakiwa alikuwa na mashahidi watatu waliotoa ushahidi wa kumtetea.

Inadaiwa katika utetezi, mshtakiwa alikana kumtukana mama yake na anadai kesi ilitokana na masuala ya biashara na kwamba wanataka aondoke katika familia.

Hakimu Mpaze alisema baada ya kupitia ushahidi wa Upande wa Mashtaka, hakuona sababu ya kutoamini ushahidi wa shahidi wa kwanza na mashahidi wengine watatu wa upande huo.

"Nimeshindwa kuona kwamba ushahidi wa shahidi wa kwanza na watatu ni ushahidi wa kutengenezwa.

"Mshtakiwa alitumia maneno hayo ya kuudhi dhidi ya mama yake hadi kusababisha mama kulia," Hakimu alisema.

Aliendelea kusema mshtakiwa anatambua maneno ya kuudhi na kwamba sio rahisi kuamini kwamba mzazi alikuja mahakamani kutengeneza kesi kwa mtoto wake wa kwanza na kama kuna mgogoro wa biashara, kwa nini mshtakiwa peke yake wakati eneo la biashara lina maduka 20.

"Upande wa Mashtaka umethibitisha shtaka bila kuacha shaka. Mahakama inamtia hatiani kwa kosa aliloshtakiwa nalo," alisema.

Wakili wa Serikali, Nancy Mushumbusi, aliomba mshtakiwa apewe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine kwa kuwa ni mkosaji anayerudia makosa.

Wakili Nancy alidai mshtakiwa aliwahi kutiwa hatiani mara mbili katika Mahakama ya Mwanzo Kariakoo kwa makosa kama hayo, akaonywa na sasa ana kesi nyingine inaendelea katika Mahakama ya Mwanzo Ukonga.

Alidai mshtakiwa apewe adhabu kali kwa kuwa ametenda kinyume cha mila na desturi za Kitanzania kwa kumtukana mama yake mzazi ambaye alitoa ushahidi kwa uchungu huku akilia.

Akiomba kupunguziwa adhabu, mshtakiwa alidai ni mama mwenye watoto wanamtegemea, hajaolewa, anapitia changamoto nyingi za kisaikolojia, hivyo aliomba apewe nafasi nyingine atajirekebisha.

Hakimu Mpaze, akitoa adhabu, alisema amezingatia hoja za pande zote mbili na ameona mshtakiwa ni mkosaji wa mara kwa mara.

"Mshtakiwa angekuwa wa kubadilika, alivyotiwa hatiani asingerudia makosa. Ili iwe fundisho kwake na wengine wanaotukana wazazi wao, mahakama inakuhukumu kwenda jela mwaka mmoja gerezani," Hakimu Mpaze alihitimisha.




Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Emmanuel Tutuba na Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Anders Sjoberg, wakionyesha hati ya makubaliano ya msaada wa SEK milioni 450 sawa na Sh. bilioni 118 kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, zilizotolewa na nchi hiyo kwa ajili ya kusaidia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kupitia Mfuko wa TASAF. **PICHA: WFM**

# Sabaya kizimbani kesi uhujumu uchumi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wenzake saba leo wanatarajiwa kupandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha kusomewa maelezo ya awali ya kesi inayowakabili mahakamani huko.

Katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba 27 ya mwaka 2021, mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine ni Silvester Nyengu (26), Daniel Mbura (38), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Agosti 13, mwaka huu, Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, alidai mahakamani huko kwamba upelelezi wa shauri hilo umekamilika, hivyo kuiomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa kwa kesi hiyo ili kuwasomea maelezo ya awali washtakiwa hao.

"Mheshimiwa Hakimu, upelelezi wa shauri hili umekamilika, tunaiomba mahakama yako tukufu kupanga tarehe ya kutajwa kwa shauri kwa ajili ya kuja kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali," alidai Kweka.

Wakili huyo pia alidai mahakamani huko kwamba walikuwa katika hatua ya kukamilisha utaratibu wa kisheria ili mahakama hiyo kupewa kibali cha kusikiliza kesi hiyo kwa kuwa haina uwezo na mamlaka ya kusikiliza.

"Mheshimiwa Hakimu, tupo katika hatua ya kukamilisha utaratibu wa kisheria ili mahakama hii ipewe ruhusa na kibali cha kusikiliza shauri hili kwa kuwa kisheria haina uwezo wala mamlaka ya kusikiliza," alidai Wakili Kweka.

Baada ya maelezo ya wakili huyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Martha Mahumbuga, aliahirisha shauri hilo hadi Agosti 27, mwaka huu (leo), washtakiwa hao watakaposomewa maelezo ya mashtaka yanayowakabili.

Washtakiwa Sabaya, Nyegu na Mbura pia wanakabiliwa na kesi nyingine ya unyang'anyi wa kutumia silaha iliyopangwa kutolewa hukumu Oktoba Mosi mwaka huu katika mahakama hiyo.

# Wachungaji 17 wa KKKT wafutwa kazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO wa kuhamisha makao makuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Konde kutoka Tukuyu wilayani Rungwe kwenda jijini Mbeya, umechukua sura nyingine, baada ya uongozi wa juu wa Dayosisi hiyo kuwafuta kazi wachungaji 17, wanaopinga kuhamishwa kwa makao makuu hayo.

Katibu wa Dayosisi hiyo, Mchungaji Ikupilika Mwakisimba, aliyasema hayo jana wakati wa mkutano wa viongozi wa kanisa hilo na waandishi wa habari, ambapo alisema wachungaji hao waliasi kanisa na kuanza kutoa taarifa za uongo kuhusu kuhamishwa kwa makao makuu.

Alisema wachungaji hao waliungana na aliyekuwa Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi hiyo ya Konde, Geofrey Mwakihaba, ambaye anadaiwa kushiriki hatua zote za maamuzi ya kuhamisha makao hayo pamoja na utekelezaji wake.

Alisema baada ya mgogoro huo, uongozi wa dayosisi hiyo ulijaribu kutafuta nafasi ya kuzungumza na aliyekuwa msaidizi wa Askofu pamoja na wachungaji hao waliokuwa wanapinga kuhamishwa kwa makao makuu hayo bila mafanikio, kutokana na viongozi hao kutokuwa tayari.

Alisema wachungaji hao waliamua kuandaa waraka na matamko ya kutokuwa na imani na askofu na Halmashauri Kuu ya Dayosisi hiyo, hali ambayo iliashiria kukana ajira yao.

"Kwa mantiki hiyo, wachungaji hao walifikia hatua ya kumkana mwajiri wao, ambaye kwa mujibu wa Katiba ya Dayosisi yetu ni Dayosisi yenyewe pamoja na ukweli kwamba kazi ya uchungaji ni ya wito," alisema Mwakisimba.

Kwa upande wake Askofu wa Dayosisi hiyo alisema uamuzi wa kuhamisha dayosisi hiyo ulifanywa kwa kuzingatia Katiba ya KKKT, Dayosisi ya Konde pamoja na kufuata taratibu zote zinazoelekezwa kwenye Katiba ya Dayosisi hiyo.


Alisema uamuzi wa kuhamisha dayosisi hiyo haukufanywa na askofu peke yake wala viongozi peke yao kama ambavyo imekuwa ikipotoshwa na wachungaji, ambao aliwaita 'waasi' bali ulifanywa na Halmashauri Kuu ya Dayosisi ambayo alisema ndicho chombo cha kikatiba.

Alisema mchakato wa kuhamisha makao makuu hayo ulianza Julai mwaka 2020, na kwamba Halmashauri Kuu ilizingatia kanuni na taratibu zote za kanisa hilo.

"Ili kutimiza jambo hilo, halmashauri kuu iliundwa kamati maalumu, ambayo iliyozunguka katika majimbo yote saba ya dayosisi na kuonana na halmashauri zote za majimbo pamoja na makundi mbalimbali wakiwamo vijana, wenzi wa wachungaji, baraza la wazee pamoja na wachungaji wastaafu na elimu ikatolewa ya kutosha," alisema Askofu Mwaikali.

Alisema mgogoro huo unachagizwa na ubaguzi wa kikabila na kikanda kwa maelezo kuwa wengi wanaopinga kuhamishwa kwa makao hayo ni wa ukanda wa Busokelo, ambao hata hivyo hakutaja kabila lao.

Kwa upande wake Kaimu Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Gwamaka Mwankenja, alisema kutokana na tatizo hilo, viongozi wanakusudia kuendelea kufanya maombi, ili mgogoro huo ufikie mwisho kwa maelezo kuwa migogoro ya kidini ni mibaya.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Balozi wa Jamhuri ya Czech nchini, Martin Klepetro, baada ya kupokea hati yake ya utambulisho, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia apokea hati za utambulisho wa mabalozi 5

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alipokea hati za utambulisho wa mabalozi watano walioteuliwa kuziwakilisha nchi zao nchini.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, mabalozi waliowasilisha hati za utambulisho ni Martin Klepetko ambaye ni Balozi wa Jamhuri ya Czech nchini, mwenye makazi yake jijini Nairobi nchini Kenya na Maria Alejandra, ambaye ni Balozi wa Jamhuri ya Chile nchini, mwenye makazi yake pia jijini Nairobi nchini Kenya.

Wengine ni Pavel Vziatkin, Balozi wa Jamhuri ya Belarus nchini mwenye makazi yake jijini Nairobi nchini Kenya na Luke Joseph Williams ambaye ni Balozi wa Australia nchini mwenye makazi yake jijini Nairobi nchini Kenya na Monica Greiff Lindo, Balozi wa Jamhuri ya Colombia nchini mwenye makazi yake jijini Nairobi nchini Kenya.

Akizungumza baada ya kupokea hati hizo ikulu jijini Dar es Salaam, Rais Samia aliwapongeza mabalozi hao na kuwaomba kufikisha salamu zake kwa viongozi wakuu wa nchi hizo na kusisitiza kuwa Tanzania ipo tayari kuendeleza uhusiano na ushirikiano kwa manufaa ya pande zote.

Kwa upande wao, mabalozi hao walimpongeza Rais Samia kwa utendaji mzuri na kumuahidi ushirikiano.

## Zitto aahidi maboresho TCD

**Na Christina Mwakangale**

MWENYEKITI wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Zitto Kabwe, ameahidi kuhakikisha kwa kipindi cha miezi sita mazingira ya kufanyia kazi ya watumishi na wadau wa kituo hicho yanaboreshwa na kukirudisha kwenye hadhi yake.

Amesema kituo hicho ambacho hutumiwa na viongozi wakuu wa kisiasa katika kujadiliana na kutafuta mwafaka wa masuala ya kitaifa, kitajengewa uwezo na kuaminika kwa wadau wake.

Zitto aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam jana baada ya kuchukua nafasi ya uenyekiti kutoka kwa aliyemaliza muda wake, James Mbatia, Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi.

Alisema atafanya maboresho ya ufanyaji kazi wa TCD kwa kuondoa upungufu wake wa sasa, kujaza nafasi za kiutendaji zilizo wazi ikiwamo ya mkurugenzi na kuboresha ushirikishaji kwa vyama vingine ambavyo havina uwakilishi bungeni kwa lengo la kutanua wigo wa ufanyaji kazi.

"Tutaitumia TCD kama gari jipya la kujenga msingi wa ujenzi mpya wa demokrasia yetu iliyodumaa, hasa baada ya uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

"Hili litahusisha kujenga upya uwezo wa vyama kujiendesha, kujenga kuaminiana, kujenga taasisi zilizo huru na zinazoaminika za kusimamia uchaguzi na siasa zetu, kuifanya TCD kuwa mhimili wa majadiliano ya wadau wa siasa, kuyatumia majadiliano kama msingi wa kupata Katiba Mpya pamoja na kuwa na mabadiliko ya kimsingi kwenye uendeshaji wa siasa zetu," aliahidi.

Zitto alisema kuwa ili kuyafanya mambo hayo, kunahitaji ushirikiano mkubwa kati yao na viongozi, vyama na watendaji wa TCD.

Vilevile, alibainisha kuwa watapitia hesabu za TCD, kuboresha uwezo wa ndani wa uwajibikaji kwenye matumizi ya fedha zake, kushughulikia madeni ya TCD na kujenga uwezo wa taasisi kujitegemea kifedha na uhusiano na wadau pamoja na wafadhili.

"TCD ina changamoto nyingi sana, kama hali yake ya sasa ilivyoelezwa hapa na Kaimu Mkurugenzi wake pamoja na mwenyekiti anayemaliza muda wake.

"Ni fursa kwetu wadau wa siasa kuitumia kujadiliana na kutafutia mwafaka wa mambo mbalimbali yanayotuunganisha ama kututenganisha, ni taasisi muhimu sana kwa taifa letu," alisema.

# 'Wanaopata ujauzito warejeshwe shuleni'

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa elimu wameiomba serikali kufanya mapitio ya sheria, sera na miongozo ya elimu, ili kuwawezesha wanafunzi wa kike wanaopata ujauzito wakiwa shuleni, kurudi tena kuendelea na masomo yao baada ya kujifungua.

Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TENTMET), Ochola Wayoga, alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa mkutano wa wadau hao waliokutana kwa siku mbili kujadili suala hilo, jijini Dar es Salaam.

Alisema katika utafiti waliofanya mikoa tisa nchini, wamebaini tatizo kubwa linalochangia wanafunzi wengi kupata ujauzito shuleni ni umbali mrefu wanaotumia kwenda na kurudi shuleni na umaskini, ambao huchangia wengi wao kushawishika kupewa vizawadi vidogo na kujiingiza kwenye ngono zembe.

Sababu nyingine alisema ni kubakwa wanapokuwa wanatembea kwenda na kurudi shuleni, ndoa za kulazimishwa pamoja na kukosekana kwa elimu ya afya ya uzazi kwa wanafunzi hao.

"Na ndio maana tukakutana wadau wa elimu kwa siku mbili kujadiliana na kuiomba serikali iangalie kwa jicho la pili suala hili, kwa sababu kuendelea kuwazuia watoto hawa kurudi shuleni baada ya kujifungua ni kuendelea kukaribisha umaskini, pia kuendelea kuongeza idadi ya watoto wa kike wasio na elimu," alisema Wayoga.

"Na ndio maana tunaiomba serikali iliangalie hili haraka kwa sababu hata huko vituo vya kutolea elimu (QT) wanaofanikiwa kwenda ni wale wachache wenye uwezo wa kulipia kwa sababu ni gharama kubwa na walioko mijini tu, je kwa wasio na uwezo na waliko vijijini?" Wayoga alihoji.

Alisema hakuna sheria au sera mahususi inayosema mwanafunzi akipata ujauzito anatakiwa kufukuzwa shule isipokuwa kinachotumika ni mapokeo tu.

# Viongozi waonywa kuchonganisha wananchi

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAKUU wilaya za Korogwe na Lushoto mkoani Tanga, wameonya viongozi wa serikali za vijiji kuacha kuwachonganisha wananchi katika masuala ya mipaka kutokana na maslahi yao binafsi.

Wakuu hao Basila Mwanukuzi wa Korogwe na Kalisti Lazaro wa Lushoto, walitoa onyo hilo juzi baada ya kufanya mkutano katika kitongoji cha Kwebamba ambako kumeibuka mgogoro wa mpaka baada ya kugundulika madini aina ya Silicon.

Lazaro alisena wananchi kwenye shughuli zao hakuna mipaka lakini hapa wanachonganishwa na wenyeviti wa vijiji kutokana na maslahi yao ya madini, viwanja na mashamba.

"Hivi hapa nani ana mgogoro wa mtu wa Mtoni Bombo, nani ana mgogoro na mtu wa kijiji cha Kalalani? Viongozi acheni kuchonganisha wananchi kwa maslahi yenu ili waanze kugombana," alisema Lazaro.

Naye Mwanukuzi alisema hakuna sababu ya watu kugombana wakati Tanzania hakuna mipaka kwa sababu wote wanatakiwa kuendesha shughuli zeo kwa kuzingatia misingi ya sheria.

Wakuu hao wa wilaya waliwaagiza wakurugenzi na wakuu wa idara za halmashauri za Bumbuli na Korogwe kufanya vikao haraka kwa ajili ya kutoa mapendekezo ili kumaliza mgogoro huo.

Gazeti hili wiki iliyopita lilitoa taarifa kuwa kugundulika kwa madini aina ya Silicon katika kitongoji cha Kwebamba kumezua mvutano wa mpaka kwa wananchi wa wilaya za Lushoto na Korogwe huku kila wilaya ikidai kiko upande wake.

Kutokana na mvutano huo, hali ya amani ilianza kuvunjika baada ya baadhi ya wakazi wa Korogwe kuanza kuwatishia maisha wananchi kwa mapanga pindi wanapowakuta kwenye mashamba ambayo wamegawiwa na serikali ya kijiji.

Diwani wa Milingano, Peter Leonard, alisema kata yake ina vitongoji 22, kikiwamo kitongoji cha K webamba na kwamba aligombea akiwa anakitambua kitongoji hicho kuwa kiko ndani ya Halmashauri ya Bumbuli, Wilaya ya Lushoto.

"Tunashangaa kuzuka kwa mgogoro huu wa kimpaka wakati inaeleweka wazi ramani ya eneo la kitongoji cha Kwebamba ambalo sasa limeingia kwenye mgogoro baina ya pande hizo mbili, imechorwa tangu kipindi cha mkoloni," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Bumba, Afizai Daffa, alisema serikali ya kijiji hicho ilianza utaratibu wa kugawa maeneo ya wazi kwa wananchi mwaka jana kwa ajili ya kuendesha shughuli za kilimo.

Alisema wananchi wa Kwebamba kuendesha shughuli za kilimo kumekuwa na changamoto kutokana na kutishiwa maisha na kikundi cha watu kutoka wilaya ya Korogwe wakiambiwa ni wavamizi jambo ambalo linatishia kuvunjika kwa amani katika kitongoji hicho.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipata maelezo kuhusu uchambuaji wa pamba kutoka kwa Emmanuel Njalu (kushoto), ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda cha kuchambua pamba cha NGS Investment Company Ltd, baada ya kuzindua kiwanda hicho, kilichopo Ifukutwa, wilayani Tanganyika, Mkoa wa Katavi, jana. **PICHA: OMR**

# Ujenzi Bandari Karema wamkuna Majaliwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amekagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa Bandari ya Karema na kusema ameridhishwa na ubora na hatua iliyofikiwa.

Majaliwa aliyasema hayo juzi baada ya kukagua mradi huo unaojengwa katika kata ya Karema Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kwa dhati kuhakikisha miradi yote inayoendelea na mingine inayoanza inakamilika kwa wakati.

Mradi huo, alisema utakuwa kiunganishi cha usafirishaji wa mizigo na abiria katika bandari hiyo na bandari ya Karemie iliyoko Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

"Nimefurahi kusikia mradi huu umefikia asilimia 50 na ifikapo Machi, mwakani, utakuwa umekamilika na tayari kwa matumizi, hivyo nawaomba wananchi mchangamkie fursa ya uwepo wa mradi huu," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Erick Hamiss, alisema ujenzi wa mradi wa bandari ya Karema umefikia asilimia 50 ya utekelezaji.

Alisema ujenzi wa mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 47.97, ulianza Agosti, 2019 na unatarajiwa kukamilika Machi, mwakani. Mradi huo umeajiri watu 300 kati yake raia wa kigeni ni tisa tu.

"Mradi huu ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi nchini hususan katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Tanganyika na nchi jirani za Zambia, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, alisema mkoa umejipanga kuzitumia vizuri fursa zitokanazo na ujenzi wa mradi huo kwa ajili ya kukuza uchumi.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kwa haya Jeshi la Polisi lijitathmini

**JUZI** Rais Samia Suluhu Hassan, aliweka bayana kilio cha wananchi dhidi ya utendaji kazi wa askari polisi kwa kubambikia kesi raia, kuwekwa mahabusu kwa muda mrefu, kutokutenda haki na kuwatesa wanapokuwa mikononi mwao.

Rais aliyataja baadhi ya mambo ambayo ni lazima Jeshi la Polisi liyaangalie kwa jicho jingine na ambayo amekuwa akiyarudia kwa zaidi ya mara tatu kuwa ni kubambikia watu kesi na kuwaacha wateseke kwa muda mrefu bila sababu.

Aidha, alisema ucheleweshaji wa upelelezi unaongeza mzigo mkubwa kwa serikali kuweka mahabusi jela. Alilitaka jeshi hilo kuangalia kesi ambazo wanaona upelelezi wake hautokamilika, watuhumiwa watolewe jela wakafaidi uhuru wao wakiwa nje.

Alitolea mfano wa nchi nyingine duniani kwamba mtu hakamatwi mpaka upelelezi umetimia, lakini kwa Tanzania hali ni tofauti kwa kuwa wapo wanaokaa kwa muda mrefu.

Tunamshukuru Rais kwa kutambua haya ambayo kimsingi ni kilio cha muda mrefu cha wananchi dhidi ya Jeshi la Polisi nchini, licha ya kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda raia na mali zao, lakini inaingia doa kutokana na matendo ambayo huumiza wananchi.

Wapo watu wanaosota rumande kwa zaidi ya wiki mbili kwa kunyimwa dhamana, huku wengine wakisota rumande kwa miaka na miaka, sababu kubwa ni kutokamilika kwa upepelezi. Hata hivyo, baadhi ya kesi zinaendeshwa kwa haraka, jambo ambalo linaonyesha iwapo kutakuwa na uwajibikaji, kesi zinaweza kukamilishwa kwa wakati.

Uwapo wa maabusu wengi una athari kwa mhusika na familia yake pekee, bali pia kwa taifa kwa kuwa ni gharama kubwa kuwatunza kuanzia chakula na huduma nyingine za kijamii.

Gharama hizi zingeweza kupunguzwa ikiwa upelelezi utafanyika kwa wakati na itasaidia serikali kuondokana na mzigo wa kuhudumia watu ambao wangeweza kuzalisha mali.

Lakini kuendelea kubambikia kesi, kunyanyasa na kuwaumiza watu na kuwasababisha vifo kwa namna yoyote ile kunaendeleza chuki na visasi visivyo vya lazima.

Yapo matukio ya ndugu kulalamika na mengine kuthibitishwa kuwa wamepoteza maisha wakiwa mikononi mwa polisi kutokana na kipigo kikali, huku baadhi ya askari wakiwajibishwa juu ya hayo, lakini yameendelea, hivyo kuchafua taswira ya jeshi hilo.


Rais amerudia mara kadhaa na sasa ameshauri kufanya mabadiliko ya sheria kuhakikisha haki inakuwapo kwa kuwa kila anayetuhumiwa ana haki hadi pale Mahakama itakapothibitisha makosa yake, na hata akihukumiwa kuna haki zake pia.

Ni muhimu Polisi likajisafisha dhidi ya malalamiko ya muda mrefu kuwa badala ya kuwa msaada sasa wamegeuka kuwa maumivu, kiasi cha watu kuona hakuna sababu ya kwenda polisi pale jambo linatokea kutokana na imani zilizojengwa au kujengeka miongoni mwa wananchi.

Tupo kwenye dunia ya utandawazi ambayo watu wanapata mambo mengi kwenye mitandao ya kijamii, ni muhimu sana Jeshi la polisi likajisafisha kwa kuondoa wanaolichafua kwa kurejesha imani kwa wananchi kuwa wao ni kimbilio na siyo sehemu ya maumivu kwa wale waliokwisha umizwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Ester Mgidula

## Tozo haikwepeki ila elimu ilikosekana

**KWA** sasa licha ya kuwa kuna mambo mengi ya kiserikali ambayo ni gumzo lakini suala la tozo za simu na kodi ya majengo bado lipo midomoni mwa watu wengi na itachukua muda kuliondoa kwenye mitandao ya kijamii.

Kabla sijaendelea kwanza nitoe pole kwa wote kwa tukio la ufyatuaji risasi lililosababisha kupoteza maisha ya Watanzania wenzetu akiwamo mhusika wa tukio hilo.

Hakika halikuwa jambo jema kwa taifa hili hatujazoea kuona matukio kama hayo kwenye ardhi hii. Naamini serikali na vyombo vya ulinzi vitachunguza na kuujua ukweli na kuhakikisha kuwa hayatokei tena.

Nikirejea kwenye mada kuhusu tozo za simu na kodi za majengo, iliyotambulishwa hivi karibuni, ikapokelewa kwa hisia tofauti huku asilimia kubwa hasa wananchi wa kipato cha chini wakiichukulia tofauti.

Kwa ufupi ni kuwa ilionekana kama tozo imekuja kuwanyonya Watanzania walio wengi, wanaotegemea simu kutuma fedha zao kwa upande wa simu.

Lakini malalamiko kwa wapangaji kuwalipia kodi ya majengo wenye nyumba.

Lakini baada ya ufafanuzi wa hapa na pale kutoka kwa baadhi ya viongozi imeonekana kama siyo jambo baya kama linavyozungumzwa na wengi, lakini liliingizwaje kwenye akili au maisha ya Watanzania? Hapo ndipo tatizo lilipoanzia.

Utafiti unaonyesha kuwa wale waliofanikiwa kusafiri kwenye mataifa tofauti wanakiri kuwa suala la kodi ni kila kila kitu, kodi hizo za wenzetu ndizo ambazo zinawasaidia kujenga uchumi wao na hata kutoa misaada kwa nchi maskini.

Tanzania ina kodi nyingi lakini huu ujio wa 'kodi za kizalendo' au tozo umeibua mengi na kuonyesha namna ambavyo watu hawakuridhia.

Wenzetu mataifa yaliyoendelea kodi zinatumika kutimiza matarajio ya wengi maana hata wale ambao hawana ajira ni rahisi kusaidia au kupata msaada kutoka serikalini.

Hapa kwetu kodi zinatumika kwa maendeleo, lakini kwa miaka mingi kumekuwa na malalamiko dhidi ya matumizi ya kodi hizo ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG) ikielezea jinsi wachache wanavyokula kama mchwa fedha za serikali ambazo ni kodi za Watanzania.

Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan umekuja na mkakati kama wanaofanya mataifa mengine wa tozo maalum za kizalendo kuboresha baadhi ya sekta.

Kama kweli makato ya tozo yataendelea kutumika ipasavyo kama serikali ilivyoahidi ni wazi basi tozo itakuwa na tija kwa wengi.

Serikali inaeleza wazi kuwa mabilioni ya fedha yaliyopatikana kwa njia ya tozo yatatumika kuneemesha idara mbalimbali za kijamii.

Hivyo, pamoja na mazuri yote hayo bado ukweli unabaki palepale kuwa elimu ingetolewa mapema kusingekuwa na maswali mengi kuliko majibu.

Hata kama mchakato unaendelea bado serikali haijachelewa, inaweza kuendelea kukusanya makato ya tozo, lakini ikitambua kuwa kuna watu wengi wameathirika kiuchumi kwa ujio wa kodi za kizalendo.

Waathirika wakubwa hapa ni wafanyabiashara wadogo wadogo waliokuwa wakitegemea wanahamisha fedha ndogo ndogo ambao wamekimbia kufanya miamala kukwepa tozo.

Kwa wananchi wenye vipato vya chini wanajijua kuwa asilimia kubwa ya matumizi yao ya kutuma na kupokea fedha wamekuwa wakifanya kwa njia ya simu.

Hiyo ilichangia kukawa na ongezeko kubwa la wafanyabiashara wanaotuma na kupokea miamala, ndiyo maana kama elimu ingetolewa mapema, basi watu wangejiandaa kwa kuwa wangejua kuchangia tozo ni kuchangia maendeleo yao.

Hatuwezi kuendelea kuangalia mataifa ya wenzetu kila siku yakiwa na maendeleo makubwa huku sisi tukisubiri hata vyoo vya shuleni kujengwa na wahisani.

Huu ni mwaka 2021, tumeshapita kule ambapo tulikuwa tunaamini kuwa maendeleo ya kweli yapo Ulaya au Amerika, kwani teknolojia imesaidia dunia kila mmoja kujitambua.

Hivyo, Watanzania waelimishwe zaidi, kuhusu umuhimu wa kutoa kodi na njia bora za kuchangia maendeleo yao.

HABARI KITAIFA

# 500 kushiriki mkutano kimataifa uwajibikaji

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya WAJIBU imeandaa Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (ITAC) unaotarajiwa kufanyika Novemba 18-19 jijini Arusha ukihusisha washiriki zaidi ya 500 kutoka ndani na nje ya nchi.

Washiriki hao wanatarajiwa kutoka taasisi za serikali, wadau wa maendeleo, wanadiplomasia, wabobezi wa masuala ya uwazi na uwajibikaji na Asasi za Kiraia (AZAKI).

Akizindua mkutano huo jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Ludovick Utouh, alisema washiriki watashiriki moja kwa moja na wengine kwa njia ya mtandao.

Utouh ambaye aliwahi kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, alibainisha kuwa kutakuwa na mada tano ikiwamo uwazi wa kifedha na uwajibikaji kama nyenzo za nchi za Afrika kufikia maendeleo ya ushindani katika uchumi.

Mada ya pili ni uhuru wa ofisi za ukaguzi za nchi na athari zake kwenye uwazi na uwajibikaji katika mabadiliko kwenye kanuni na mazoea ya ufanyaji ukaguzi wa ndani na nje.

Zingine ni uwazi na uwajibiji wa serikali za Afrika katika kushughulikia janga la corona (COVID-19); ufanisi wa TEHAMA katika kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa fedha na rasilimali za umma barani Afrika na kuwa wazi zaidi na kuwajibika na mipango ya ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi (PPP) katika sekta ya uzinduaji barani Afrika.

"Pamoja na mada hizo tano zilizotajwa hapo juu, kutakuwa na mada sita za ziada ambazo zitatolewa na kujadiliwa.

"WAJIBU pia inatarajia kutoa fursa kwa washiriki kutembea Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) kwa siku moja ili kufurahia na kushirikisha washiriki kuwa mabalozi wa kutangaza vivutio vya utalii," alisema.

Utouh alibainisha kuwa washiriki wa mkutano huo watapaswa kujisajili kwenye tovuti ya taasisi hiyo na kulipia gharama za ushiriki kulingana na makundi ya washiriki wa ndani na nje ya nchi.

Alibainisha kuwa washiriki wa ndani watalipia Sh. 400,000 na wa nje Dola za Marekani 400 (washiriki watakaohudhuria Arusha), Sh. 100,000 kwa washiriki wa mtandaoni wanaotoka Tanzania na Dola 100 kwa washiriki wa mtandaoni kutoka nje ya nchi.

# Mkakati wa viwanda vya mbao waiva

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Biashara (TNBC), kupitia kikundi kazi chake cha misitu, limeshakamilisha mkakati wa uendelezaji wa viwanda vya kuhandisi mbao mbadala (EWP).

Viwanda hivyo vitasaidia kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia sekta ya misitu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kikao cha 8 cha kikundi hicho kilichofanyika Dar es salaam jana na kuazimia mkakati huo, Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alisema maazimio ya mkutano wa 12 wa Baraza chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ulielekeza kuandaliwa mkakati wa utekelezaji wa mpango EWP.

"Tuliunda kikosi kazi kilichofanya utafiti ambao umefanikisha uandaaji wa mkakati wa utekelezaji wa mpango wa EWP ili kuanza utekelezaji wake ambao utaleta faida kubwa kwa nchi," alisema Dk. Wanga.

Alieleza kuwa sekta ya misitu ina fursa kubwa katika kutengeneza ajira pamoja na kuiletea nchi fedha za kigeni, hivyo kupitia mkakati huu tutakwenda kuibua fursa zilizopo kwa wananchi na kuzalisha ajira nyingi kupitia sekta ya misitu.

"Utekelezaji wa mpango huu ambao utasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, utachochea uanzishwaji wa viwanda vingi vya kuhandisi mazao ya misitu, jambo litakalopunguza uagizaji wa mbao mbadala kutoka nje ya nchi," alisema.

Alieleza kuwa nchi imekuwa ikipoteza fedha nyingi kwa kuagiza mbao mbadala kutoka nje ya nchi, hivyo mpango wa EWP utasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya misitu kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi na hata kuuza nje ya nchi.

"Nchi yetu ina malighafi nyingi kwenye sekta ya misitu kuzalisha mbao mbadala kulinganisha na nchi nyingine za jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), hivyo kwa kuanza uzalishaji tutajiwekeza uhakika wa soko katika EAC na mataifa mengine," alisema Dk. Wanga.

Aidha Dkt. Wanga alisema Baraza kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii litaendelea kutekeleza maazimio ya yaliyoafikiwa ambayo kwa kiasi kikubwa yapo kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano ijayo ili kuleta matokeo chanya kwenye kuliongezea Taifa kipato pamoja na kukuza uchumi wa nchi.

"Sisi kama TNBC tumeazimia kutekeleza kwa vitendo maazimio na maagizo ya serikali ambapo sekta ya misitu ni miongoni mwa sekta zilizoainishwa kwenye Mpango wa maendeleo ya Taifa wa Miaka mitano ili sekta hii iweze kushiriki kikamilifu kwenye kuliingizia Taifa faida," alisema.

Mwenyekiti wa Kikundi Kazi cha Misitu, Dk. Ezekiel Mwakalukwa, alisema serikali imejipanga na itaendelea kutengeneza mazingira mazuri ya kuboresha sekta ya misistu nchini ili kuchochea ukuaji wa sekta zingine kama ya viwanda, jambo ambalo litailetea tija taifa na kuongeza fursa za ajira nchini.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara(TNBC), Dk. Godwill Wanga (kulia), akizungumza katika kikao cha nane cha kikundi kazi cha misitu kilichoundwa na baraza hilo, jijini Dar es Salaam jana, kwa lengo la kuandaa mkakati wa uendelezaji wa viwanda vya kuhandisi mbao mbadala (EWP) zitokanazo na mazao ya misitu ikiwa ni utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa 12 wa TNBC uliooongozwa na mwenyekiti wake ambaye ni Rais Samia Suluhu Hassan. Katikati ni Mwenyekiti wa Kikundi kazi hicho, Dk. Ezekiel Mwakalukwa na Mwenyekti Mwenza wa Kikundi kazi hicho, kutoka sekta binafsi, Ben Mfungo Sulus. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Wakulima wapewa mbinu ya mazao bora

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

SERIKALI imewataka wakulima nchini kuzalisha mazao kwa tija, kwa kuzingatia ubora, kwa mahitaji ya soko la ndani na nje.

Agizo hilo lilitolewa na Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omary, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, wakati wa uzinduzi wa duka la pembejeo za kilimo la One Acre Fund, katika Kata ya Igima wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe.

Alisema serikali imedhamiria kwa dhati kuleta mabadiliko kwenye sekta ya kilimo, ikiwamo upatikanaji wa pembejeo kwa wakati.

Alisema serikali inaendelea kuboresha huduma za ugani kuhakikisha usalama wa chakula na lishe unakuwapo, ikiwamo kuhakikisha wakulima wote waliofikiwa na pembejeo za ugani wanajikita katika kilimo cha mazao yenye tija.

Aidha, alisema Wizara ya Kilimo ipo tayari kushirikiana na wadau wote wa kilimo katika kuendeleza sekta hasa katika uboreshaji na upatikanaji wa pembejeo, utafiti, huduma za ugani, umwagiliaji, miundombinu na masoko.

Aidha, alisema wakulima wanapaswa wakijiunga na kujisajili katika vyama vya ushirika, ili kuwasaidia kufikiwa na watoa huduma wengi zaidi kwa fursa mbalimbali zilizopo katika kilimo.

Alilipongeza shirika la One Acre Fund kwa kuboresha huduma zao hasa kwa kupunguza gharama za tozo katika utoaji wa mikopo ya pembejeo, kwa wakulima kutoka asilimia 19 hadi asilimia 10 kwasasa.

"Suala lingine, niwapongeze kuhusu ufunguzi wa maduka haya 30 ya huduma za pembejeo katika Mkoa wa Njombe, Mbeya na Songwe," alisema Judica.

Mkurugenzi Mkuu wa One Acre Fund Tanzania, Jennifer Lindgren, alisema katika kipindi cha miaka nane ya shirika hilo, wamejifunza kuwa wakulima wadogo wanaweza kuondokana na umaskini kama watafuata njia bora za kilimo cha kisasa.

Mkurugenzi msaidizi wa uendelezaji wa mazao masuala ya pembejeo na ushirika kutoka Wizara ya Kilimo, Beatus Malema, alilishukuru shirika hilo kwa utaratibu wa kuweka maduka ambayo yatakwenda kwa wakulima moja kwa moja, ili kurahisisha upatikanaji wa pembejeo jirani na maeneo yao.

## Ma-RC watwishwa zigo kuhusu lishe

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu, amewataka wakuu wa mikoa kusimamia suala la lishe kwa watoto ili kupunguza kiwango cha watoto milioni tatu wenye udumavu katika maeneo mbalimbali nchini.

Licha ya kutoa agizo hilo, Ummy ameipongeza baadhi ya mikoa iliyofanya vizuri kwa kutenga Sh. 1,000 za halmashauri kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana katika mkutano wa tathmini wa utekelezaji wa mkataba wa lishe nchini uliowakutanisha wakuu wa mikoa 26 wa Tanzania Bara na makatibu tawala.

Alizitaka halmashauri 11 kati ya 184 zilizoshindwa kufanya vizuri katika eneo la lishe kujieleza.

"Matumizi ya fedha za lishe yameongezeka kutoka asilimia 22 mwaka 2019 hadi kufikia asilimia 57 mwaka 2020/2021 na wakuu wa mikoa nawaombeni taarifa zinazotolewa ziwe sahihi na zenye uhalisia lengo kuondoa changamoto ya udumavu nchini," alisema Waziri Ummy.

Katika mkutano huo, alitoa vyeti kwa halmashauri tatu na mikoa mitatu zilizotumia fedha zote na kutekeleza shughuli zote za lishe kwa asilimia 100.

Alitaja halmashauri hizo kuwa ni pamoja na Mlele, Geita na Masasi na mikoa iliyofanya vizuri ni Mbeya, Ruvuma na Mtwara.

Mkuu wa Kitengo cha Lishe TAMISEMI, Mwita Waibe, alisema kuwa watoto milioni tatu chini ya umri wa miaka mitano wamedumaa sawa na asilimia 32.

Alisema ushirikishwaji na vikao vilifanyika katika mikoa mbalimbali lakini tatizo lipo kwenye kutenga fedha kupitia halmashauri.

"Kwa utafiti uliofanywa hapa ulimwenguni kwenye mabara saba takwimu zinaonyesha kuwa watoto milioni 151 wamedumaa na Afrika ni asilimia 59 na Tanzania ni asilimia 32 hivyo tunatakiwa kuhakikisha changamoto hii inaondoka," alisema

# Jengo la mama na mtoto Sekou Toure sasa kukamilika Desemba

**Na Richard Makore,** MWANZA

UJENZI wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza ya Sekou Toure, umefikia asilimia 83 ya ukamilishaji wake.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni na Meneja wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) Mkoa wa Mwanza, Bernad Mayemba, alipozungumza na waandishi wa habari katika ukaguzi wa jengo hilo uliofanywa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima.

Mayemba alisema ubunifu na ujenzi wa jengo hilo umefanyika kwa mfumo wa usimamizi na kwa kuzingatia ubora wa vifaa ambavyo vimetumika.

Alisema wako katika hatua za mwisho za ukamilishaji na wanatarajia hadi kufikia Desemba, mwaka huu, jengo hilo lianze kutoa huduma.

Pia alisema ili kufanikisha kukamilisha ujenzi huo kwa muda uliopangwa, wataongeza kasi ya kufanya kazi usiku na mchana.

Katika siku ya ukaguzi wa jengo hilo, Waziri Gwajima alisema wabunifu wa jengo hilo wamezingatia ubora na pia wamefuata ramani ambayo inaonyesha jengo lina ghorofa sita.

Aliahidi kufikia Desemba jengo hilo litakuwa limekamilika na kuanza kutoa huduma kwa mama wajawazito pamoja na mtoto.

Alisema Sh. bilioni 6 zimepitishwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kumalizia ujenzi huo.



Mjumbe wa Baraza la Uongozi wa Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA), CPA Ally Bukuku akifungua semina ya wahasibu na wakaguzi wa hesabu, inayohusu mabadiliko ya sheria za kodi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Eneo uwekezaji ladaiwa kuwa maficho ya wafugaji, wahalifu

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

ENEO lililotengwa kwa ajili ya Bandari ya Bagamoyo pamoja na la EPZA linaelezwa kuwa kificho cha wafugaji ambao wanakaa hapo na baadaye kupitisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima katika Kata ya Zinga.

Hali hiyo inaelezwa kuwa kero kwa wakazi wa kata hiyo wilayani Bagamoyo na kusababisha kuwa na kesi zisizoisha kati ya wakulima na wafugaji.

Akizungumza na Nipashe jana, Diwani wa Zinga, Mohamed Mwinyigogo, alisema eneo kubwa la kata hiyo ni bandari na eneo la viwanda ambalo wafugaji wanatumia kujificha huko.

"Wafugaji wanazidi kuingia kwa wingi katika maeneo hayo na wameweka kambi. Ukiwaendea wanasema ni aneo la serikali si la watu binafsi. Kero hii nimeifikisha kwa Mkuu wa Wilaya aishughulikie kwa nafasi yake," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Zinga, Aziza Matumla, alikiri kupokea kesi tatu kwa wiki hususani msimu wa kilimo zinazohusiana na wakulima na wafugaji.

Alikiri uwapo wa jamii ya wafugaji katika eneo la serikali la Mamlaka ya Ukanda wa Uzalishaji (EPZA) na lililotengwa kwa ajili ya bandari ambao wanatumia pori lililopo sasa kujificha na baadaye kupitisha mifugo maeneo ya wakulima.

Matumla alisema suala hilo atamfikishia Mkuu wa Wilaya ili alishughulikie kwa kuwa wafugaji hao wamekuwa chanzo cha migogoro isiyoisha katika kata hiyo.

"Katika eneo la Mlingotini, wafugaji wanapitisha mifugo yao mara kwa mara. Wapo wanaokamatwa na wakifanyiwa tathmini wanalipa wengine hawajulikani kwa kuwa hawakai hapo na wakati mwingine wakulima wanakuwa hawapo shambani," alisema.

Mtendaji huyo alisema atazungumza pia na wafugaji kuwaelekeza wasipitishe mifugo yao eneo la Mlingotini kwa sababu wamekuwa wakiharibu mazao na kusababisha hasara kwa wakulima

Ramadhani Gubi, mmoja wa wakazi wa Mlingotini, alisema kila wanapolima mpunga, ng'ombe wanakula, hivyo wanapata mavuno hafifu na wakati mwingine hawavuni kabisa.

Mkazi mwingine wa Mlingotini, Mtengani Said, alisema wafugaji wamekuwa wakilisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima kwa makusudi na kwamba maisha yao yako hatarini kwa kuwa baadhi yao wamefanyiwa vitendo vya kikatili.

# NIC yazipa shule 50 vikoti angavu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC) mkoani Shinyanga, limetoa msaada wa vibao na vikoti angavu kwa shule 50 kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi kuongoza vyombo vya moto kusimama katika maeneo ya vivuko.

Vifaa hivyo vitasaidia wanafunzi kuongoza vyombo vya moto kusimama kwenye vivuko ili kukabiliana na ajali za wanafunzi barabarani.

Meneja wa shirika hilo mkoani Shinyanga, Hamis Mohamed, akizungumza juzi wakati wa kukabidhi vifaa hivyo kwa Jeshi la Polisi, alisema lengo la msaada huo ni kuzuia ajali kwa wanafunzi wanapokuwa wakivuka barabara.

Alisema wametoa vibao 150 vyenye kuonyesha ishara ya 'stop, go' na vikoti angavu 100, ambavyo vitasaidia wanafunzi kuongoza vyombo vya moto wanapokuwa wakivuka barabara kwa kuvisimamisha ili wavuke salama na kuepuka ajali.

"Tumekabidhi vibao na vikoti angavu vyenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa Jeshi la Polisi, ambavyo vitapelekwa shuleni ili visaidie kuzuia ajali za barabarani kwa wanafunzi mkoani Shinyanga.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Joseph Paul, alisema vitakuwa msaada katika kukabiliana na tatizo la ajali za wanafunzi wanapokuwa wakivuka barabara.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Shinyanga, Malege Kilakala, alisema kabla ya kuvikabidhi vifaa hivyo shuleni, watatoa elimu kwanza kwa wanafunzi namna ya kuvitumia wakati wa kuvuka barabara kwenye vivuko.

# Taasisi sasa kupigia debe kilimo alizeti

**Na Sabato Kasika**

MWENYEKITI mstaafu wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Ruangwa, Nachingwea na Liwale (RUNALI), mkoani Lindi, Hassan Mpako, ameanzisha taasisi iitwayo Liwale Social Economic Development Organization (LSD-Organization), itakayokuwa na kazi ya kuhamasisha kilimo cha alizeti.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema taasisi hiyo imepata usajili wenye namba 08NGO/R/ 2137 ambayo alikabidiwa hivi karibuni na ofisi ya msajili wa asasi za kiraia jijini Dodoma.

Mpako alisema, kwa sasa taasisi hiyo inaundwa na watu wanne aliowataja kwa majina ya Hashimu Majangagara (mwenyekiti), Ally Kamuna (katibu mkuu), Said Mulila (mwenya hazina) na yeye kama mkurugenzi wa uhamasishaji.

"Tumeanzisha taasisi hii ya kuhamasisha kilimo cha alizeti kina faida, kwa kuwa mafuta yake yanahitajika kwa wingi, ndani na nje ya nchi, lakini kinachukua muda mfupi kati ya miezi mitatu hadi minne tu kuanzia kupanda hadi kuvuna," alisema Mpako.

Alisema, taasisi hiyo itazinduliwa rasmi mwanzoni mwa mwezi ujao, kisha itaanza kazi ya uhamasishaji wa kilimo cha zao hilo, ili liwe na umaarufu kama ilivyo korosho, ufuta na mbaazi.

# Mashine 73 za michezo ya kubahatisha zateketezwa

**Na Richard Makore,** MWANZA

BODI ya Michezo ya Kubahatisha nchini imeteketeza mashine 73 za michezo ya kuhabatisha ambazo hazijasajiliwa.

Aidha, imewaonya maofisa utamaduni na michezo wa wilaya kuacha tabia ya kutoa vibali kwa wamiliki wa mashine hizo bila kufuata utaratibu.

Mkurugenzi Mkuu wa bodi hiyo, James Mbalwe, aliyasema hayo jana jijini Mwanza aliposimamia uteketezaji wa mashine hizo katika dampo la Buhongwa.

Alisema jukumu la kutoa vibali kwa ajili ya biashara ya michezo ya kubahatisha ni la bodi na siyo chombo ama mtu yeyote nchini anayeweza kufanya kazi hiyo.

Aliongeza kuwa maofisa utamaduni na michezo wameamua kujitwisha jukumu ambalo siyo la kwao kisheria, na kwamba wanasababisha kuzagaa kwa mashine hizo katika maeneo ambayo hayaruhusiwi.

Mbalwe alisema mashine zote zinatakiwa kusajiliwa na kuwekewa alama maalum pamoja na kuwekwa sehemu za baa na siyo mtaani kila kona.

Alifafanua kuwa wanapata taarifa mbalimbali katika maeneo ya nchi ambazo zinawasaidia kukamata mashine hizo ambazo hazina viwango, usajili na ambazo zimewekwa maeneo yasiyoruhusiwa.

Kwa upande wake, Meneja wa Ukaguzi na Udhibiti kutoka bodi hiyo, Sadik Elmusu, alisema licha ya michezo ya kubahatisha kusaidia kuongeza mapato ya serikali, lakini hawawezi kuruhusu ifanyike kiholela.

Elmusu alisema mpaka sasa kwa nchi nzima wamesajili mashine 25,000 na kwamba moja inaingiza Sh. 110,000 kwa mwezi.

Alisema mashine hizo zilizoteketezwa zilikuwa zinaingiza mapato ya serikali yanayofikia Sh. milioni 96 kwa mwezi.

Mashine hizo ziliharibiwa kwa kupondwa kwa kutumia 'tinga tinga' katika dampo la Buhongwa jijini Mwanza.



Katibu wa Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA), Kanda ya Kaskazini, Godwin Jeremiah (kushoto) na Ofisa Msimamizi wa chama hicho Arusha, Mohamed Mpinga, wakitoa elimu kwa abiria ya jinsi ya kutambua haki zao na kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona katika stendi kuu ya mabasi, jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KACU yang'ara kimataifa ubora pamba

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

CHAMA Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Kahama (KACU) kimesema kuwa kimeanza kufanya biashara ya zao la pamba na mataifa ya Ulaya, kutokana na ubora wa pamba hiyo.

Pamba hiyo inachakatwa na kiwanda chake kilichopo Kata ya Mhongolo, hali ambayo inaonyesha kuwahamasisha wakulima kuendelea kulima zao hilo.

Kimesema kwa sasa zao hilo linaonekana kuwa na tija kwa wakulima nchini kutokana na kampuni za nje kulipenda zao hilo na kuanza kulinunua kwa wingi.

Kaimu Meneja Mkuu wa chama hicho, Abdul Ally, akizungumza na waandishi wa habari, alisema kiwanda kimezalisha robota 3,200 za pamba nyuzi na mbegu 600,000, na kwamba robota hizo pamoja na mbegu zina wateja wa mataifa ya nje.

Alisema pamba nyuzi iliyozalishwa kiwandani hapo tayari ina wateja wanne, mteja mmoja ni Uturuki, wateja wengine watatu ni wa ndani wakiwamo Afeshian na MO.

"Niwaombe wakulima wasikate tamaa waendelee kulilima zao hilo kwa kuwa tayari tumeanza kupata wateja kutoka nje ya Tanzania," alisema na kuongeza:

"Na katika kilimo hicho wajitahidi kulima pamba iliyo bora kwa kuzingatia viuatilifu na wakati wa uvunaji watumie maturubali ili pamba iwe safi, kwani itaongeza ubora wenye tija kwa wateja wetu."

Pia, alisema kuwa licha ya changamoto ya kubadilika holela ya kwa bei ya pamba, KACU imejipanga kununua kilo milioni 6 za pamba katika Halmashauri za Wilaya ya Ushetu, Kahama, Msalala, Nyang'hwale Mkoa wa Geita, Kishapu mkoani Shinyanga na Meatu mkoa wa Simiyu.

"Hapo awali kulikuwa na changamoto kubwa sana ya pamba, na changamoto kubwa ni kupanda kwa bei ya pamba mbegu kila uchao nchini, asubuhi unaweza kuamka na kukuta bei ni Sh. 1,200, mchana ikawa 1,300-1,500, kama KACU tulianza na bei ya Sh. 1,100 baada ya bei elekezi ya shilingi 1,050 iliyotolewa na Bodi ya Pamba, sisi tukaongeza Sh. 50," alisema Ally na kuongeza:

"Lakini hadi kufikia leo, sisi KACU pamba tunainunua kwa bei ya shilingi 1,550 kwa kilo, lakini kwa sasa tumejikita kuinunua kwa wilaya za Kishapu na Meatu, kwa sababu maeneo ya Nyang'hwale na Kahama pamba imekwisha, na hata hivyo, kulingana na changamoto ya uchache wa pamba, KACU tumejipangia kununua kilo milioni 3.5 kama itapatikana."

# Makalla aja na dawa uhaba wa madarasa

Na Christina Mwakangale

MKUU wa Mkoa Dar es Salaam Amos Makalla, amesema kutokana na ongezeko kubwa la watu mkoani Dar es Salaam, mkakati uliopo hivi sasa ni majengo ya shule za umma kuwa ya ghorofa ili kukabiliana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Kwa mujibu wa tovuti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), mkoa huo una jumla ya shule za sekondari za umma 133 za msingi zikiwa 355, huku sensa ya mwaka 2012 ikibainisha idadi ya watu ni 4,364,541.

Makalla aliyasema hayo jana katika moja ya redio, akizungumzia masuala mbalimbali ya kielimu, kiuchumi na mikakati ya kimkoa.

Alisema ongezeko la wakazi jijini linasababisha ardhi kuwa na matumizi makubwa, hivyo ujenzi huo utasaidia eneo moja kuwa na madarasa ya kutosha.

"Tunatarajia majengo ya shule za umma Dar es Salaam kuwa ya ghorofa kutokana na ongezeko la mahitaji ya shule, ardhi mahitaji yake yameongezeka hivyo mpango ni kubadili mwonekanao wa majemgo haya," alisema Makalla.

Alibainisha kwamba, mbali na hilo, mpango mwingine ni kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuwa na usalama kwa kuhakikisha kila barabara ya kiwango cha lami inakuwa na kamera za CCTV, ili kurekodi matukio yote yanayotokea barabarani na kuongeza hali ya usalama.

"Tayari kuna watu wameanza kuonyesha nia ya kufunga taa, kuiweka Dar es Salama, miundombinu mizuri na biashara itaweza kufanyika saa 24, mahali popote kwenye uhakika wa usalama kuna biashara muda wote," alisema Makalla.



Rais Samia Suluhu Hassan (kulia), akiteta jambo na Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubo na Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Aikansia Muro (kushoto), baada ya kufungua kikao kazi cha Jeshi la Polisi cha Mwaka, jijini Dar es Salaam juzi, kilichodhaminiwa na benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka kamati kusimamia mapato

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, amewaelekeza wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo, kuwa sehemu ya kusimamia vyanzo vya mapato kwenye halmashauri ili kubaini uhalali wa makusanyo kwa mwezi.

Wajumbe hao ni wakuu wa wilaya, madiwani na wakurugenzi watendaji wa halmashauri za mkoa huo. Shigela ametoa uamuzi huo wakati wa kikao cha kujadili mkakati wa kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2022 kilichofanyika Manispaa ya Morogoro.

Alisema mapato yanayokusanywa na viongozi ambao wamepewa dhamana ya kusimamia vyanzo hivyo hayaendani na matarajio ya halmashauri hali inayochangia kushuka kwa mapato kila mwaka.

Aidha, alitolea mfano wa kituo cha mabasi Msamvu kilichopo Manispaa ya Morogoro kinachokusanya Sh. milioni tatu kwa siku zinazotokana na mabasi yaendayo mikoani, kwamba ni ndogo ikilinganishwa na mabasi yanayopita pamoja na shughuli nyingine ambazo zinafanyika katika kituo hicho.

"Mapato ya kituo kikuu cha mabasi cha Msamvu bado ni madogo mimi nakuunga mkono Mstahiki Meya, nenda na kamati yako katika kituo cha mabasi Msamvu mkasimamie mapato, hata Kamati ya Ulinzi na Usalama ruksa," alisema Shigela.

Katika hatua nyingine, aliwaagiza wakuu wa wilaya, wenyeviti wa halmashauri na wakurugenzi watendaji mkoani humo kusimamia miradi yote inayotekelezwa katika maeneo yao na kutoa taarifa juu ya maendeleo ya miradi hiyo ili kuisaidia serikali.

Awali, akizungumzia suala la upotevu wa fedha zinazotokana na mapato ya Halmashauri Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Mariam Mtunguja, aliagiza watendaji wanaohusika katika ukusanyaji wa fedha hizo kisha wakazitumia kinyume na utaratibu wafikishwe mahakamani.

Hata hivyo, alisema, kabla ya viongozi hao kufikishwa mahakamani watalazimika kulipa pesa hizo na endapo hawatakuwa nazo mali zao zitauzwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Malinyi, Pius Mwelase, alisema hatua ya Shigela kuruhusu madiwani wa halmashauri hiyo kushiriki kusimamia mapato itasaidia kuchangia kuvuka kwa lengo la halmashauri katika ukusanyaji wa mapato.

Mwelesa alisema kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wamekusanya takriban Sh. milioni 216 kwa mwezi Julai kutoka Sh. milioni 40 hadi 50 zilizokuwa zinakusanywa kwa mwezi.

# Jamii yaomba elimu chanjo ya COVID-19

Na Yasmine Protace

IMEELEZWA kuwa changamoto za kijinsia zinachangia wanawake wengi hasa waliopo pembezoni mwa miji kutopata elimu sahihi juu ya chanjo, ambayo inatolewa kwa sasa duniani kwa ajili ya kukabiliana na maambukizi ya corona.

Mbali na serikali kupitia wadau wa afya, kuhamasisha watu kuchanja kwa hiari, lakini bado baadhi ya wanawake wameonekana kuachwa nyuma kwa sababu ya kutokuwa na elimu sahihi ya chanjo hiyo.

Hayo yalisemwa jana katika Semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS) na Salome Luben, mwenyekiti wa kikundi cha wanawake Mashujaa Machimbo Kata ya Kipunguni mkoani Dar es Salaam.

Salome ambaye ni mjumbe katika kamati ya wazazi katika Shule ya Sekondari Kipunguni, alisema serikali za mitaa zitumike kutoa elimu ya chanjo ya corona ili wanawake wengi zaidi wakiwamo na wa pembezoni waweze kunufaika na elimu hiyo.

"Elimu ipo kupitia vyombo mbalimbali vya habari juu ya chanjo, lakini tukumbuke wanawake wengi ni watafutaji, hawawezi kusikiliza vyombo vya habari kwa wakati kutokana na kuwa katika mihangaiko ya kutafuta riziki," alisema.

Aliongeza kuwa watendaji wa vijiji ikiwamo na kata watumike kuitisha mikutano, huku wakiwa na wataalamu wa chanjo, na kwamba hali hiyo itasaidia elimu kuyafikia makundi yote.

Janet John, mshiriki wa GDSS, alisema mitazamo ibadilike kwa jamii kuhusiana na suala la chanjo badala ya kuiona kuwa ni kwa ajili ya mtu ambaye anataka kusafiri.

"Baadhi ya watu mitazamo yao ni mibaya katika chanjo, ingawa kuchoma ni hiari. Lakini baadhi mitazamo yao wanadhani wanaotakiwa kuchoma ni wasafiri tu," alisema.

Alishauri kwamba elimu ya chanjo iendelee kutolewa ili jamii ielewe.

Akizungumzia mlengo wa kijinsia katika suala zima la chanjo, alisema baadhi ya wanawake hususani wa pembezoni wako zaidi katika utafutaji na hivyo kusikiliza vyombo vya habari juu ya chanjo, wanakosa muda au wengine kutokuwa na redio au TV na kusoma gazeti hajui.

"Ili wanawake wanufaike na chanjo hiyo ambayo ni ya hiari, inatakiwa viongozi wa serikali za mitaa waitishe mikutano ili wazungumze na wanawake juu ya chanjo ya corona," alisema.

**"Elimu ipo kupitia vyombo mbalimbali vya habari juu ya chanjo, lakini tukumbuke wanawake wengi ni watafutaji, hawawezi kusikiliza vyombo vya habari kwa wakati kutokana na kuwa katika mihangaiko ya kutafuta riziki," alisema.**



Corona ilivyowaletea neema wanakijiji mbegu za mahindi Ukurasa 14



Darasa la wanawake wauza dagaa DRC

Ukurasa 12

BUFE

IJUMAA AGOSTI 27, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

ESTHER LEMA:

# Kutoka kuuza lita moja ya asali hadi kusafirisha tani kadhaa nje ya mipaka

**Na Sabato Kasika**

HATA mbuyu ulianza kama mchicha, ndivyo imeweza kuwa kwa Esther Lema, ambaye anafanya biashara ya kuuza asali maeneo mbalimbali nje na ndani ya nchi, huku akimiliki mizinga 600 ya nyuki mkoani Tabora.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili, Esther mwenye miaka 33, anasema, alianza biashara hiyo kwa mtaji wa Shilingi 40,000, kwa kununua lita tano za asali na kutembeza mitaani na sasa amefikisha mtaji wa Shilingi 6,000,000.

Lakini leo anazungumzia biashara kubwa ya asili inayovuka mipaka kutoka Tanzania hadi Somalia na ndoto yake ni kulitawala soko la Afrika Mashariki kuanzia Dar hadi Nairobi na pia Congo.

Katika mazungumzo yake na gazeti hilo, anasema alianza biashara hiyo mwaka 2019 baada ya kuacha kazi ya kushona nguo aliyoifanya kwa miaka sita jijini Dar es Salaam na kuongeza: "Niliamua kubadili kazi baada kuona ushonaji unachelewesha kufikia malengo ya kuinua kipato changu, ndipo nikajaribu biashara ya kuuza asali nikianzia na dumu la lita tano," anasema Esther.

Anafafanua kuwa alinunua dumu la asali la lita tano kwa Sh. 40,000 na kuigawa katika chupa za lita moja, ambapo kila lita aliuza kwa Shilingi 12,000, na kwamba aliuza kwa siku moja na kuimaliza.

"Nilinunua nyingine ya lita tano nayo ikaisha, ikabidi ninunue dumu la lita 20 ambalo nilikaa nalo kwa muda wa siku mbili nalo likaisha, nikaongeza jingine nikaendelea kufanya hivyo kwa miezi nane," anasema.

Esther anasema, baada ya kuona biashara ya asali inazidi 'kuchanganya', akapata wazo la kwenda mwenyewe Tabora kuifuata huko na kuachana na mtindo wa kuagiza watu wamletee na kuongeza:



Esther Lema akiwa na kifaa maalum cha moshi wa kufukuzia nyuki wakati wa kurina asali



Baadhi ya mizinga yake anayomiliki

"Niliamua kusafiri kwa treni hadi Malongwe mkoani Tabora ambako asali inapatikana kwa wingi, nilikuwa sipajui, sina ndugu, lakini nikaamua kwenda, ili nitimize lengo la kufanya biashara."

Anasema, akiwa ndani ya treni, alikutana na mzee mmoja na kumweleza kile kinachompeleka huko na kumwelekeza sehemu ambayo asali inapatikana kwa wingi, ambapo walishuka naye.

Licha ya kuhofia usalama wangu, kwani tulishuka saa tisa za usiku kwenda nyumbani kwa mzee huyo huko Malongwe, kumbe ni mtu mwema tu, tulifika nikanunua asali madumu mawili ya lita 20 kutoka kwa watoto wake," anasema.

Akiwa na mtaji wa Shilingi 200,000 , alidhani dumu la lita 20 ni Sh. 100,000, lakini anabahatika kulinunua kwa watoto hao kwa Sh. 70,000 kila moja na hivyo kubakiwa na Sh. 60,000, na kurudi Dar es Salaam kuendelea kuuza na kusafiri hadi Malongwe kununua nyingine kila ilipokwisha, lakini baadaye mmoja wa watoto wa mzee huyo alimshauri amiliki pori na kuweka mizinga yake.

**AMENUNUA PORI**

Anasema, alinunua pori lenye zaidi ya eka 10 kwa Sh. 500,000 na kuanza na mizinga 100, na kwamba kadri mambo yalivyochanganya, aliongeza mingine na sasa ana jumla ya mizinga 610.

"Baada ya kuwa na mizinga yangu, niliachana na mtindo wa kununua asali kwa wauzaji wengine, badala yake ninarina yangu mwenyewe na kwenda kuuza maeneo mbalimbali nchini," anasema.

Anasema, katika mizinga hiyo, anaweza kuvuna mapipa matano hadi sita ya asali, na kwamba uvunaji hufanyika mara mbili kwa mwaka Februari na Juni na anatumia wafanyakazi wake watano aliowaajiri kwa kazi hiyo.

"Biashara ya asali imebadili maisha yangu, kutoka mtaji wa Sh.40,000 hadi kufikia Sh. milioni sita, pia nimefanikiwa kujenga nyumba Mbezi Makabe na ninasomesha watoto wangu wawili kwenye shule za kulipia,"anasema.

**MALENGO YAKE**

Esther anataja baadhi ya malengo yake kuwa ni kuongeza mizinga hadi kufikia 2,000, kuwa na duka la kuuza asili Afrika Mashariki na kuwa msambazaji bidhaa hiyo kwa wateja wengi eneo hilo.

"Ninatarajia kupanua soko zaidi kwani nimekuwa nikiuza asali Dar es Salaam Arusha na Nairobi Kenya na sasa nimepata wateja kutoka Somalia, hivyo sina budi kupanua zaidi biashara yangu na kuvuka mipaka ya Afrika Mashariki," anasema.

Aidha anasema, anajipanga kuhamasisha mabinti wengine kufanya biashara ya asali kwa kuwa inalipa na kwamba kuna kipindi inaadimika ambapo dumu la lita 20 linanunuliwa kwa Sh.160,000 hadi 170,000.

"Msimu unapokuwa mzuri, dumu la lita 20 za asali huuzwa kati ya Sh 80,000 hadi 100,000, ikiadimika ndipo bei inapanda hadi kufikia 170,000, hivyo mtu akiwa na mizinga kidogo, inaweza kubadili maisha yake kwa kuiuza kwa faida kubwa hasa wakati inapoadimika," anasema.

UCHUMI

# Darasa la wanawake wauza dagaa DRC

## ■Waambiwa itumieni SIDO, H/shauri ■Wanunuzi wenu wasiingie 'jikoni'

**Na Mwandishi Wetu**

"NATAKA kutoka kimaisha, lakini mambo ni magumu. Biashara ya dagaa haijaweza kutufikisha kule tunapopata. Kwa miongo mingi tumeuza dagaa , lakini nyumba zetu ni duni.Angalia ni za makuti na udongo."

Anasema Fatuma Machalila, mkazi wa Kilwa Masoko, mkoani Lindi, ambaye mapema mwezi huu anatembelewa na wanahabari kufahamu mafanikio na changamoto kwenye biashara ya dagaa inayofanywa na kinamama wengi wilayani humo.

Anasema biashara hiyo haijatengamaa kwani hawana soko la uhakika mnunuzi mkubwa wa dagaa zao ni wafanyabiashara wa Congo, lakini hawajaweza kunufaika kutokana na kukosa mitaji, teknolojia na miundombinu duni wanayotumia kukausha samaki hao.

Mwanamama huyo, anawaambia wanahabari wanaotembelea mafanikio ya kazi za kuhamasisha wanawake kujiinua kiuchumi inayofanywa na SHirika la Action Aid Kilwa, kuwa wanakausha dagaa kwa jua kwenye vichanja na msimu wa mvua hakuna jua, hali ni mbaya zaidi, anasema mwanamama huyo aliyeanza biashara hiyo, 1993.

Pia anasema hawana utaalamu wa kuzichambua kimadaraja, kuzifunganya na kuweka lebo, ili zifike sokoni zikiwa zimeongezewa thamani.

Fatuma ni miongoni mwa wanawake wengi Kilwa waochakata mazao ya samaki, wanaiona kuwa ni pasua kichwa.

Wanaeleza kuwa kinachowakwamisha ni kukosa mitaji hivyo wanasubiri 'tajiri' kutoka Congo, awape 'oda' na kuwaachia fedha za kufanyia kazi hiyo na wanachofanya ni mbinu za kupata fedha kidogo baada ya kuandaa shehena ya mteja.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake anasema, wanakosa teknolojia na miundombinu ya kufanikisha mnyororo mzima wa biashara hiyo, kuanzia wanapowatoa baharini hadi kumuuzia mteja.

Ili kufahamu namna ya kuwasaidia, Nipashe inazungumza na Ofisa Miradi na Mchambuzi wa Sera, kutoka Shirika la Usimamizi wa Mazingira na Uchumi (EMEDO), Lawrence Kitogo , ambalo pia hufanyakazi na kinamama wachakataji wa mazao ya samaki,



Fatuma Machalila, akionyesha jiko na teknolojia duni inayotumiwa kuchemsha dagaa na chumvi kabla ya kuwakausha waitwao dagaa nyama kazi inayofanyika Kilwa. Jiko hilo hutumia kuni na si rafiki wa mazingira.

anaeleza mambo ya kuwasaidia.

Anasema mtandao wa wanawake wanaochakata mazao ya samaki umesambaa maeneo mengi, wako baharini, maziwani kama Victoria, Tanganyika, Nyasa, mtoni mfano Kilombero na Mtera, pia wapo kwenye mabwawa kama Nyumba ya Mungu.

Anasema tatizo kubwa ni kukosa miundombinu na teknolojia ya kuchakata kuanzia ya kuvua dagaa majini, upokeaji bidhaa hiyo wavuvi wanapofika pwani, vibebeo, vifaa vya kuwasafishia, kuchuja maji, kuwakausha, kuwachambua, kuwaweka kwenye madaraja, kuwafungasha na kuweka lebo.

Kitogo anasema baadhi ya wajasiriamali wanaochakata mazao hayo wanakosa teknolojia hiyo.

Anataja mathalani, ubebaji hufanyika kwenye ndoo za kawaida, lakini kuna matenga ya plastiki maalumu ya kubebea dagaa.

Kitogo anafafanua kuwa dagaa wanaanikwa kwenye chanja, lazima ziwe za kisasa siyo kutumia vyandarua au nyavu za mbu zinazowekwa madirishani na kufunikwa na nailoni au maturubai.

"Vichanja kama sehemu ya miundombinu vinahitajika viwe vya kisasa vya kupokelea, kuchambulia ili kuondoa taka kama uduvi, konokono na taka bahari. Vichanja vya kuchambua na kutofautisha ukubwa navyo ni muhimu. Vingine ni vya kuzikaushia maji na kuanikia kwa kutumia teknolojia ya kisasa," anaelezea Kitogo.

Ofisa Miradi na Mchambuzi wa Sera, kutoka EMEDO anasema kina mama hao ni wanachama wao na kwa Tanzania nzima, kuna mashirika zaidi ya 260 ya vikundi vya wafanyabiashara hao zaidi ya 2,000 wanaochakata mazao ya samaki.

" Wapo wanaoshughulika na dagaa kwenye maji ya chumvi baharini mathalani Kilwa na Tanga, wengine wapo kwenye maji madogo haya ni mabwawani na mtoni na wapo kwenye maji ya baridi ndani ya maziwa mbalimbali kama Victoria na Tanganyika, ambao kwa kukosa miundombinu wanapata matatizo haya."

Akizungumzia athari za wafanyabiashara kuwafuata wachakataji nyumbani na kuwapa mitaji na `oda' au kuruhusiwa kufika kwenye kambi za wavuvi na kutoa maelekezo ya kile wanachotaka siyo biashara endelevu.

"Wafanyabiashara wanatakiwa wafike sokoni tu. Siyo kwenye kambi za wavuvi wanapokwenda huko wanaweza kununua bidhaa bila kuwa rekodi. Biashara hiyo inazikosesha halmashauri na mamlaka za mapato mapato na takwimu sahihi za bidhaa na ushuru. Wabanwe kwa kutumia sheria, ili wafuate utaratibu."

Anataja hasara nyingine kuwa wajasiriamali hao wanashindwa kuchakata kwa viwango vya kufungasha na kuweka lebo na kuuza kwa uzani unaokubalika kama gramu na kilo.

"Kukosa vipimo rasmi kunasababisha wapate hasara ya kuuza kiwango kikubwa kwa gharama ndogo.

Ikumbukwe kazi ya kuchakata inaanzia kuwatoa baharini hadi kuwauza kwa mteja, ikipitia hatua nyingi. Tena wanauza dagaa wakavu, lazima kuwe na utaratibu bora wa kuuza kwa mteja wa mwisho, ili kupata faida na si hasara."

"Wanapata hasara baada ya mavuno `post harvest loss`

Iwapo hakuna ufungashaji na lebo makini wanunuzi wanaweza kufungasha upya na kuziongezea thamani bidhaa hizo na kupata faida kubwa zaidi hasa inapokwenda nje ya nchi."

Mazao ya samaki kama dagaa na vibambara au makayabo yanaelezwa kuwa yanatokea Congo husafirishwa nje ya nchi na kufikishwa mji wa Matonge huko Ubelgiji, pia huuzwa katika miji mingine ya Afrika, licha ya kwamba nchi hiyo haina bahari.

### UFUMBUZI UNAOPENDEKEZWA

Kitogo ambaye shirika lao linashughulikia mazingira ikiwa ni pamoja na bahari, maziwa na mito, misitu na ardhi, anashauri Wizara ya Mufugo na Uvuvi na halmashauri iwawekee miundombinu na teknolojia ya kukaushia iwe ya gesi, umeme na jua, ili waachane na kuni. Moshi unaharibu bidhaa hizo.

"Iweke viwanda vidogo vidogo, vyenye vichanja, vya kusafisha, kuchambua, kuangalia wakubwa na wadogo, kuchemsha, kukaanga, kukausha, kufunganya kwenye uzito mbalimbali na kuweka lebo..."

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ione kama ni hitaji la kinamama wengi na ichukue hatua.

### UHIFADHI NI MUHIMU

Akizungumzia namna ya kuboresha soko hilo mchumi na mtafiti Dk. Deogratias Lwezaura, anasema pamoja na kupewa utaalamu wa kisasa wa biashara hiyo, wachakataji hao wa mazao ya samaki watafanikiwa iwapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na halmashauri zitawapatia teknolojia inayoanzia kuwavua majini hadi kuwaweka lebo na kuwauza, ili wafanye shughuli zao kisasa kwa faida zaidi. "Juhudi hizi ziende pamoja na kuwapatia sehemu za kuhifadhi 'cold rooms' wahifadhiwe kwenye majokofu kila wanapovua, ili kila wakati dagaa wapatikane kusiwe na madai kuwa hawapo, kwa sababu ya upepo au mvua."

Anashauri kuwa katika uwekezaji huo, vikundi visaidiwe kila kimoja kiwe na lebo yake, ili vifanyekazi kwa utaalamu na kwa ushindani zaidi kuongezea dagaa thamani na kujielekeza kwenye ufanisi zaidi.

Dokta Lwezaura Meneja Mipango na Tathmin wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo TARI-Dodoma, anakumbusha kuwa katika biashara hiyo hakuna haja ya kuwa na mwekezaji mkubwa, badala yake wizara na halmashauri ziwawezeshe wajasiriamali, ili kuinua uchumi wa watu wa chini na kubadili maisha yao.

Anasema kupitia mikopo ya halmashauri ya vijana , wanawake na watu wenye ulemavau hilo linaweza kufanyika. Anasema hayo alipoulizwa iwapo wanaweza kutafutiwa wawekezaji wakashirikiana nao.

### SIDO YAWASHAURI

Mhandisi Profesa Sylivester Mpanduji ni Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), anasema teknolojia za ukaushaji dagaa zipo na zinatumiwa na wanaochakata mfano Mwanza, Kigoma na hivi karibuni wamepokea maombi kutoka kwa wajasiriamali wa Zanzibar.

Anaongeza kuwa wanatoa mafunzo ya kuboresha uchakataji dagaa, ukaushaji na kufunganya kitaalamu na kwamba SIDO Lindi, inaweza kuwasaidia kwenye eneo hilo.

Anataja teknolojia hizo kuwa ni ya kukausha kwa nishatijua na nyingine ni ya mkaa kidogo inayotumia feni zinazotoa upepo mwingi kukausha dagaa hizo kwa ufanisi.

Anawashauri wachakataji hao kama tatizo ni mitaji kuomba fedha za halmashauri kupitia mikopo ya wanawake , wenye ulemavu na vijana pamoja mikopo ya SIDO kwa vile suala hilo limeshapatiwa ufumbuzi.



Mayasa Kasie mfanyabiashara wa dagaa anayetamani teknolojia bora ya ukaushaji yenye vichanja vilivyoboreshwa na ukaushaji unaofanyika mwaka mzima. **PICHA ZOTE: MWANDISHI WETU.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Kweli ipo haja kufupisha majina






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

KUNA moja kati ya makabila zaidi ya 120 nchini, ambalo lina majina marefu, lakini linafahamu fika namna ya kuyafupisha, ili kupunguza kibarua cha mtu kuyatamka, na hatimaye kutamkika kirahisi zaidi. Wenye majina yao marefu wanajijua na mikoa yao.

Hili la kuyafupisha kwa mfano mtu anaitwa Kinenekejo anafupishwa kuitwa Kejo, nalipongeza, kwa sababu matumizi ya maneno mafupi wakati mwingine hurahisisha watu kutamka na kuandika, hivyo kuepuka kufanya makosa katika hilo.

Na hii ilisumbua sana kwani mwaka jana kwenye uchaguzi mkuu kuna wagombea waliwekewa mapingamizi kwa kukosea majina yao.

Lakini hili la majina marefu linaendelea mpaka kwenye majina ya wizara zetu nchini, zina mambo mengi na marefu kiasi kwamba mtu kutamka jina la wizara mathalan, inakuwa shida na katika kuandika ndiyo kabisaa, yanakosewa. Unajiuliza kwa nini basi!

Hebu kwa mfano, Wizara ya Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Hii ni mifano michache tu, hivi kwa mfano unakuwa na Wizara ya Afya tu, humo ndani ukakuta hayo mengine ya wanawake, sijui watoto na nini! Kwani hao wanawake na watoto hawana afya? Kwa nini nao wanatajwa tofauti?

Hivi ikiwa Wizara ya Ulinzi tu na Jeshi la Kujenga Taifa ikawa humo ndani kuna tatizo? Au ikaitwa tu Wizara ya Majeshi-yaani Jeshi la Wananchi likawa ndani, Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na JKT, kuna tatizo?

Hebu angalia, mathalan sisi wa vyama vya wanahabari siku moja tukasema tunaandaa tukio maalumu ambalo tutahitaji mgeni rasmi aje na awe ni Waziri wetu, tutamwita nani na mwingine asilalamike kutengwa?

Tuna Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa; yupo Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile.

Bashungwa atataka kuja kwa sababu anasimamia habari lakini Ndugulile anayesimamia redio na televisheni asije?

Kwa nini hizi wizara mbili zisitenganishwe, mathalan Bashungwa akabaki na ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, huku Habari ikahamia kwa Ndugulile? Mbona rahisi tu na kazi ikaendelea?

Angalia, tuna wizara inayohusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, aliko Ummy Mwalimu, humo kuna mambo ya afya na elimu, lakini kuna Wizara ya Elimu aliko Profesa Joyce Ndalichako, kuna Wizara ya Afya aliko Dorothy Gwajima, wanapishana wapi?

Nimesema hii ni mfano tu, wizara zote zikiangaliwa kwa umakini, tutabaini kuwa ipo haja ya mabadiliko na marekebisho, kwa kupunguza wingi wa wizara na kubakiwa na chache tena zenye majina mafupi.

Mama ana nafasi ya kufanya hivyo, kipindi hiki ambacho anakuna kichwa kupata mbadala wa marehemu Elias Kwandikwa katika Wizara ya Ulinzi, ambayo anaweza kuiita Wizara ya Majeshi, kwani si lazima kuiga nchi zingine.

Ndiyo sababu pia, si lazima uwe na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kana kwamba Afrika Mashariki si nje ya nchi! Kwani ikiwa ya Mambo ya Nje tu haitoshi? Ngoja tumwache Rais Samia Suluhu Hassan akune kichwa na hatimaye aje na timu yake.

Tumeimaliza hiyo, sasa tutarudi kwenye majina ya shule zetu za msingi na hata sekondari, ambazo utakuta vibao vyao au hata barua zao zikiandikwa kwa kuanza na Wizara ya Elimu, Halmashauri ya Wilaya ya Watu , Shule ya Msingi Maendeleo , Sanduku la Posta 800, Mikocheni, Konondoni, Dar es Salaam.

Hapo hujaambiwa ni shule ya kutwa au ya bweni. Kibao barabarani kinakuwa kimejaa maandishi mpaka kusoma kunahitaji mtu ashuke kwenye gari akajisomee, kama anajiandaa kwa mtihani! Turekebishe! Alamsiki!

UCHUMI

# Corona ilivyowaletea neema wanakijiji mbegu za mahindi



Mahindi ya njano ni nafaka yenye kiwango kikubwa cha wanga na virutubisho ikilinganishwa na meupe. Jamii hii hulimwa kwa wingi maeneo ya Korogwe mkoani Tanga. **PICHA: MTANDAO**

**Na Jenifer Gilla**

AKIELEKEA kumaliza kuvuna mahindi katika shamba lake lililopo kilomita tano kutoka nyumbani kwake, Toba Athumani (60) haamini anachokiona. Anahakikisha kwa kuangalia mashamba ya majirani, kujiridhisha iwapo macho yake hayadanganyi.

Mkazi huyo wa Kijiji cha Kwakombo katika Halmashauri ya Mji Korogwe, mkoani Tanga anafurahishwa na wingi wa mavuno ni mara mbili ya mwaka jana, kwa kiasi kile kile cha mifuko nane ya mbegu ya mahindi kwenye heka moja.

"Miaka ya nyuma nilikuwa nikivuna magunia 35 ya mahindi kwa heka tano, wastani wa magunia saba kwa heka, mwaka huu nimepata magunia 75 kila heka moja nimevuna magunia 15... zamani nilikuwa nasomba mara mbili nikitumia trekta safari ni mara nne,"anasema na kutabasamu.

Mkulima huyu mwenye familia ya mke na watoto wawili, anaona mfumo wa maisha yake ukibadilika kutokana na mazao mengi na kujihakikishia kipato kuongezeka mara mbili zaidi na kujiweka katika hali salama ya uhaba wa chakula.

"Mauzo yakienda vizuri ninategemea kupata takriban Sh. 3,000,000. Iwapo nitauza kila gunia kwa Sh.40,000, hela ninayoitumia kuihudumia familia yangu ikiwa ni pamoja na kulipa ada za watoto, tofauti na mwaka jana ambapo niliambulia Sh.1, 200, 000 kwenye magunia 30, "anasema Toba.

Siri ya matumaini mapya ya kilimo kwa Athumani ni matumizi ya mbegu za kisasa zinazohimili athari za mabadiliko ya tabianchi zilizoelekezwa kwa wanakijiji wa Kwakombo.

### HALI ILIVYOKUWA

Rashidi Salim (55), ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwakombo chenye wakazi 1,700, ambao asilimia 90 wanalima mahindi kujikwamua kiuchumi, anakiri kuwa kilimo cha mahindi kilidorora.

"Kilimo cha mahindi kilikuwa kinakataa, hadi kufikia baadhi ya wakulima wakaacha, tukatoa taarifa kwa maofisa kilimo kwa sababu tuliona kijiji kinaelekea kupata njaa, tunashukuru Mungu mwaka huu wametutembelea kutuelekeza kuhusu mbegu za kisasa.

"Ofisa kilimo alituletea kilo 300 za mbegu ya DK 8031 na DK 9089, tukawapatia wakulima 75 wenye mashamba wanaolima kitaalamu tukampa kila mmoja mifuko minne inayotosha nusu heka. Kisha tukawaelekeza zinakopatikana ili wakanunue, walipanda mwezi Machi, mwaka huu na ndiyo wanavuna sasa", anasema Salim.

Mnufaika mwingine wa mbegu hizo, Athumani Ally anasema heka moja aliyoipanda mbegu ya DK 8031 ameona tofauti kubwa katika mavuno.

"Nilipewa mifuko minne nikaongeza nyingine ya 'Tumbili nikachanganya nikapanda heka moja, nimevuna magunia 14 tofauti na mwaka jana nilipata matatu ambayo hayakutosha kwa chakula na kuuza," anasema Ally.

### KUKABILI COVID-19

Mbegu hizo za majaribio, ni msaada kutoka kampuni za Agricultural Council of Tanzania (ACT) na Dayer, uliolenga kuwasaidia wanakijiji kupambana na njaa katika kipindi cha janga la COVID-19 ukijulikana kama Covid Donation 2020.

Mkuu wa Idara ya Kilimo na Umwagiliaji Halmashauri ya Mji Korogwe, Ramadhani Sekija, anasema mradi huo ulilenga kusaidia Wilaya za Korogwe mjini na vijijini, ili kuongeza chakula kwa wananchi.

"Tulipokea mbegu tani 10, na kuzigawia Korogwe mjini na vijijini kila eneo tani tano na jumla ya wakulima 1,197 wa vijiji saba na mitaa 22 wamenufaika, huku taasisi 10 na maofisa ugani 33 pia walipata mbegu hizo" anasema Sekija.

Utambulisho wa mbegu hizo ulienda sambamba na elimu inayohusu umuhimu wa kutumia mbegu hizo, kwa mujibu wa Ofisa kilimo wa Kata ya Kwamsisi, Said Sharif, wanavijiji walielimishwa kuhusu changamoto iliyopo katika kilimo kwa sasa na umuhimu wa kuhamia kwenye mbegu za kisasa zinazohimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Walieleza kuwa moja ya mbinu itakayowatoa kutoka kwenye athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye kilimo ni kutumia mbegu za kisasa. Tunashukuru wameelewa na mwamko wa kutumia mbegu za kisasa ni mkubwa " anasema Sharif.

### WAKULIMA WAHAMASIKA

Elimu kuhusu matumizi ya mbegu za kisasa imetoa hamasa kwa baadhi ya wakulima waliokuwa wamekata tamaa na kushawishika kurudi tena katika mstari wa kilimo cha biashara kama anavyoelezea Fatuma Mgolo (60).

"Nilishakata tamaa, walivyokuja kutuelimisha nikasema ngoja nijaribu, nikaenda kununua dukani nikalima heka yangu moja, aisee mazao ni mengi japo mvua zimekataa, msimu ujao nalima kibiashara kama zamani", anasema Fatuma.

### MATATIZO YALIYOIBUKA

Ingawa mbegu hiyo aina ya DK 8031 inatoa mavuno mengi inalalamikiwa kushambuliwa na wadudu hasa vidudumuzi na viwavijeshi, anasema Toba Athumani.

"Tunaiomba serikali itusaidie viuatilifu kupambana na wadudu hawa wanaoharibu mazao, mhindi unaliwa na kubakia unga,"anaongeza.

### UHAKIKA WA CHAKULA

Dokta Honest Kessy ni Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Chakula Wizara ya Kilimo, anayeihakikishia nchi kuwa ipo salama katika upatikanaji wa chakula na viini lishe lakini, anaonya haipaswi kuridhika na hali hiyo.

"Mfumo wetu wa uzalishaji upo vizuri, mwaka jana tulikuwa na tani milioni 18.2, mwaka huu tunapambana zaidi kwa kuhakikisha tunadhibiti visumbufu vya kilimo na kuhimiza kilimo cha kisasa kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, ili tuzalishe zaidi kipindi hiki cha corona, hata tukisema tujiweke 'lockdowns' tusiwe na shida ya chakula.

" Pia tunafanyia kazi upatikanaji masoko nje ya nchi, ili wakulima wetu wanufaike na wenzetu wawe na uhakika wa chakula hasa katika kipindi hiki. Mfano ule mgogoro wa Kenya kukataa mahindi ya Tanzania kuwa yana sumu kuvu tumeumaliza na wakulima wanaendelea na biashara, "anasema Dk. Kessy.

Anataja matatizo ya kilimo kuwa ni pamoja na ukame, maeneo mengi kukosa mvua za kutosha mfano mikoa ya Tanga, Arusha na Kilimanjaro.

Anataja ardhi kukosa rutuba na kuchoka baada ya kutumika muda mrefu na kuingia tindikali inayosababisha mimea kutofyonza mbolea.

### MBINU ZA UFUMBUZI

Dokta Kessy anasema Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), imepata suluhusho la kuondoa tindikali kwenye udongo kwa kutumia chokaa inayomwagwa kwenye udongo kupunguza tindikali.

Baadhi ya maeneo yaliyofikiwa na chokaa hiyo ni Mbeya na Songwe ambapo wakulima wameitumia msimu huu wa masika na wamepata matokeo mazuri, anaongeza Kessy. Ripoti ya Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) ya Matarajio ya Mazao na Hali ya Chakula (2020),inaeleza kuwa mataifa 32 kati ya 44 yanahitaji msaada wa chakula na nchi hizo ziko Kusini ya Jangwa Sahara, ikiwamo Tanzania.

Inafafanua kuwa ukame, mafuriko na majanga mengine yanaweza kuongeza upungufu wa chakula na kukwamisha kufikia lengo namba mbili la Maendeleo Endelevu (SDG 2) la kupunguza udumavu wa watoto kwa asilimia 50 ifikapo 2030.

Ripoti ya Shirika la Chakula Duniani juu ya Usalama wa Chakula, kipindi cha corona inaonyesha kuwa Tanzania ambayo ina idadi ya watu milioni 58, milioni 15 ni maskini.

Inaongeza kuwa watu 5,000,000 wanaishi chini ya mstari wa uhaba wa chakula kati yao milioni mbili wako mijini na kwamba kupungua kwa shughuli za uchumi na kijamii kutokana likizo ya COVID-19 , kutaathiri mapato na usalama wa chakula katika maeneo ya mijini.



# CCM yashtukia mpango kuuzwa gari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dodoma, kimeshtukia mpango wa kuuzwa kwa gari la serikali Toyota V8 ambalo halikuwa kwenye orodha ya magari yaliyopangwa kuuzwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

Gari hilo lilinunuliwa kwa Sh. milioni 140, lakini lilipangwa kuuzwa kwa Sh. milioni 4.9.

Kutokana na hali hiyo, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Godwin Mkanwa, ameagiza kusitishwa mpango wa baada ya kubaini halikuwa katika orodha hiyo.

Akizungumza wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo katika halmashauri hiyo, Mkanwa alisema uuzaji wa gari hilo haukuzingatia sheria.

"Hii haikubaliki, gari lile linaweza kutengenezwa. Nilipokuwa Mwenyekiti wa Halmashauri hii nilianzisha mchakato wa kununua gari lile kwa Sh. milioni 140 kwa matumizi ya halmashauri," alisema.

Mkanwa alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mwanahamisi Ally, kuhakikisha mchakato huo unasitishwa.

Pia alimwagiza mkurugenzi huyo kukifumua kitengo cha ununuzi katika halmashauri hiyo kwa kuwa kinasababisha urasimu katika ununuzi ya vifaa vinavyotumika ujenzi wa miradi ya shule na vituo vya afya.

Alitoa agizo hilo baada ya kutembelea ujenzi wa maabara katika Shule ya Sekondari Kimaghai na ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Ilolo. Baadhi ya wajumbe wa kamati za ujenzi pamoja na mafundi walilalamikia ucheleweshaji kupata idhini ya ununuzi wa vifaa.

Mkanwa alisema serikali haitaki ubabaishaji fedha zinatolewa kwa wakati lakini wapo watendaji wanachelewesha malipo na kibali cha ununuzi wa vifaa.

"Maeneo yote tuliyopita kitengo cha manunuzi kimelalamikiwa, hivyo mkurugenzi hakikisha unakifumua kitengo hiki," alisema.

Aidha, aliwataka watumishi wa halmashauri za Dodoma kuacha kusingizia kuwa mifumo ya malipo kuwa haijafunguliwa.

Mwenyekiti huyo alisema kisingizio hicho kimekuwa kigezo cha kuchelewa utekelezaji wa miradi ya maendeleo wakati serikali imekwishatoa fedha kwa wakati.

Naye Mkurugenzi Mwanahamisi Ally aliiahidi Kamati ya Siasa kuwa watatekeleza maagizo yote ikiwamo kukiimarisha kitengo cha ununuzi.

## Mbunge ataka malezi kwa manufaa ya taifa

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

MBUNGE wa Bahi, Kenneth Nolo, amewataka wazazi na walezi wa wilaya hiyo kuwajibika kwenye malezi ya watoto ili kuwaandaa kuwa viongozi bora na waaminifu kwa taifa.

Nolo alitoa ushauri huo jana alipokuwa akizungumza na wananchi katika viwanja vya msikiti wa Taqwa, Kigwe wilayani hapa.

Alisema iwapo wazazi watawajibika ipasavyo kwenye malezi na kuhakikisha wanapata elimu taifa litakuwa na viongozi bora.

"Ili taifa lipate viongozi bora na wacha Mungu, jukumu la kwanza la malezi lipo kwa wazazi na walezi ambao wanaoweza kuwawekea misingi mizuri ya elimu," alisema.

Naye Sheikh wa Wilaya hiyo, Suleimani Twalib, aliwaomba wazazi na walezi kutekeleza wajibu wao katika kuhakikisha watoto wanajengewa misingi bora ya elimu.

Alisema jukumu la kulea watoto lipo kwa wazazi na walezi, hivyo ni wajibu tena ni haki kuhakikisha elimu wanaipata bila kukosa.

Sheikh Twalib aliwahimiza wananchi kujali afya zao, badala ya kuyumbishwa na baadhi ya watu ambao wamekuwa wakipotosha uhalali wa chanjo ya corona.

**"Ili taifa lipate viongozi bora na wacha Mungu, jukumu la kwanza la malezi lipo kwa wazazi na walezi ambao wanaoweza kuwawekea misingi mizuri ya elimu," alisema.**



Sheikh wa Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma, Suleiman Twalibu, akizungumza na waumini wa dini ya kiislamu kwenye sherehe ya Maulidi, katika uwanja wa msikiti wa Taqwa, kijijini Kigwe hivi karibuni. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Sheikh ahimiza wananchi kushiriki sensa

**Na Peter Mkwavila,** MPWAPWA

WAKAZI wa Wilaya ya Mpwapwa wametakiwa kuonyesha ushirikiano kwenye sensa ya watu na makazi itakayofanyika mwakani na kuzingatia maelekezo sahihi kwa maofisa kwa ajili ya kupata taarifa.

Sheikh wa Wilaya ya Mpwapwa, Ally Salumu, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wilayani hapa.

Aliwashauri wakazi hao kutoa taarifa sahihi na za ukweli sensa hiyo kwa ajili ya kuhesabu watu na makazi itakayofanyika Agosti, mwakani.

Pia aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi muda ukifika na kutoa ushirikiano na serikali katika kujibu kwa usahihi kwa yale watakayoulizwa na maofisa hao.

"Nia ya serikali ni kutaka kujua idadi ya watu wake pamoja na makazi, hivyo ninawaomba wakazi wa wilaya hii ya Mpwapwa kujitokeza kwa wingi na kushirikiana na serikali ili lengo hilo la uhesabiaji wa watu na makazi uweze kufanikiwa kwa kupata idadi iliyo sahihi," alisema.

Aidha, Sheikh Salumu aliomba serikali kuendelea kuwatumia viongozi wa dini kufikisha elimu ya umuhimu wa kujikinga na corona ili kusiwapo na mivutano isiyo na tija.

Alisema viongozi wa dini wana nafasi kubwa ya kuwaelimisha waumini wao kujitokeza kwa wingi na kupata chanjo kwa ajili ya kujilinda na corona.

Alisema vijiji vingi wilayani Mpwapwa bado vinahitaji watu wake kuelimishwa juu ya ugonjwa huo wa corona kuhusiana na madhara yake.

"Hivyo viongozi wa dini kwa kushirikiana na wataalamu wa afya wana nafasi kubwa ya kutoa elimu itakayotosheleza kwa watu na wakaamini na kulifanikisha uchanjaji wa chanjo," alisema.





# Madereva serikali wamjia juu RPC

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU chache baada ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani kutangaza kuanza operesheni dhidi ya magari ya serikali yanayokiuka Sheria za Usalama Barabarani ikiwamo kuendeshwa kwa mwendokasi, Chama cha Madereva wa Serikali kimeibuka na kukemea vikali kauli hiyo kikidai kuwa kauli hiyo ina lengo la kuwakomoa wanachama wake.

Agosti 23, mwaka huu, baada ya kutokea ajali ya gari la serikali mkoani Songwe na kusababisha vifo vya watumishi watano wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wa mikoa ya Mbeya na Songwe, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema ameanzisha operesheni ya kukamata magari hayo ya serikali.

Kamanda Wankyo alisema jeshi lake limebaini kuwa baadhi ya magari ya serikali yanaendeshwa kwa mwendokasi kuyapita magari mengine pasipo kuchukua tahadhari na baadhi yana madeni makubwa yaliyotokana na tozo za papo kwa papo na hawataki kulipa kwa hiari.

Alisema operesheni hiyo itayahusu magari yote yenye usajili wa serikali na taasisi zake ambayo ni yenye namba za STK, STJ, STL, DFP, SM, SU na mengine yanayoendeshwa bila kutii sheria za usalama barabarani.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Serikali nchini, Flora Mnyandavile, alisema kauli ya Kamanda Wankyo haikuwa nzuri kwao na kwamba ilikuwa ikiashiria kuwa wanasababisha ajali kwa makusudi.

Alisema madereva ni kama watumishi wengine wa serikali na wakipata ajali inakuwa bahati mbaya kama inavyokuwa kwa madereva wengine, hivyo hawatakiwi kuchukuliwa kama wanasababisha ajali kwa makusudi.

Mnyandavile alisema ni vizuri Jeshi la Polisi likajikita kwenye utoaji wa elimu ya usalama barabarani kwa madereva wote badala ya kutoa kauli za kutishia na kuwakatisha tamaa ambazo alisema zinawafanya wafanye kazi kwa hofu.

"Dereva wa serikali ni mtumishi wa serikali kama walivyo watumishi wengine. Pia ikumbukwe kwamba dereva wa serikali hafanyi uamuzi wa kwenda mahali popote pasipo ridhaa ya kiongozi anayemwendesha, hivyo tunaomba matamko ya viongozi hawa yazingatie hilo," alisema.

Mwkamu mwenyekiti huyo alisema kauli ya RPC Wankyo ililenga kukwamisha shughuli za serikali kwa maelezo kuwa wao wanawaendesha viongozi wenye majukumu mbalimbali.

Katibu wa Madereva wa Serikali Wilaya ya Mbarali, Idrisa Kaberege, alisema madereva ni binadamu kama wengine, hivyo huwa hawapendi kupata ajali wanapokuwa kazini.

Alisema asilimia kubwa ya madereva wa serikali wanaendesha magari kwa umakini na kwa weledi kutokana na aina ya watu wanaowabeba na kwamba ndiyo sababu ajali zinazohusisha magari ya serikali ni chache kuliko ilivyo magari mengine.

"Kifo hupangwa na Mungu na hakuna binadamu anayependa kufa. Hata sisi madereva huwa hatupendi kusababisha ajali wala kufa. Kinachotokea huwa ni bahati mbaya kama inavyokuwa kwa madereva wengine," alisema Kaberege.

Naye Andrew Mwangunile ambaye ni Katibu wa Madereva wa Serikali Wilaya ya Kyela, alisema wakati mwingine ni kweli kwamba magari ya serikali huwa yanakimbia lakini yanakuwa na sababu maalumu ya kufanya hivyo.

Alisema wakati mwingine kiongozi anayemwendesha anapigiwa simu na viongozi wa ngazi za juu wakimtaka afike Dodoma ndani ya muda mfupi hivyo hulazimika kuendesha gari kwa mwendo mkubwa ili afike kwa muda unaotakiwa.

Hata hivyo viongozi hao wa madereva walitoa pole kwa ndugu jamaa na marafiki wa watumishi wa TRA waliofariki dunia baada ya kupata ajali wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe akiwamo na dereva mwenzao.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa moja ya majengo ya kituo cha pamoja cha Forodha kwenye mpaka wa Tanzania na Malawi wa Kasumulu wilayani Kyela, mkoani Mbeya, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wadau washiriki ujenzi madarasa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali mkoani Mbeya, imeanza kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo wakiwamo wananchi kukabiliana na uhaba wa vyumba vya madarasa kwa kujenga shule sita mpya za sekondari.

Aidha, halmashauri ya wilaya hiyo imeahidi kumaliza tatizo la baadhi ya wanafunzi hasa wanaoanza kidato cha kwanza baadhi yao kuchelewa kuanza masomo kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, aliyasema hayo alipokuwa anazungumza na Nipashe akitanabahisha kwamba wananchi wengi wamekuwa na mwamko kuunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha wanafunzi wanasoma kwenye mazingira mazuri.

Mfune alisema shule zilizojengwa kwa ushirikiano kati ya serikali na wananchi ni za sekondari za Muwale (madarasa matano), Kapunga (matatu), Itamboleo ( vyumba vitatu vya madarasa), Ihanga (vyumba vitano) na Nyamakuyu vyumba vitano.

"Ujenzi wa shule hizi ni mwendelezo wa ujenzi wa shule za sekondari na vyumba vya madarasa kwa shule zilizopo. Mwaka 2020 serikali kwa kushirikiana na wananchi tulifanikiwa kujenga shule mbili ambazo ni Ipwani na Mwakaganga," alisema Mfune.

Alisema mafanikio ya ujenzi wa shule hizo unatokana na michango ya hiari ya wananchi katika kuharakisha sekta ya elimu wilayani humo, pamoja na mipango thabiti ya wilaya katika kuondokana na kikwazo kwa wanafunzi wanaokosa elimu kwa sababu ambao zipo ndani ya uwezo wa wilaya.

# Wanafunzi walala chini kisa bweni kuteketea kwa moto

**Na Nebart Msokwa,** MAKETE

BAADHI ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Ikuwo iliyopo wilayani Makete, Njombe, wanalazimika kulala chini kutokana na mali zao ikiwamo vitanda na magodoro kuteketea kwa moto uliounguza bweni lao miezi miwili iliyopita.

Kutokana na hali hiyo wanafunzi hao wameiomba serikali pamoja na wadau mbalimbali kuwasaidia kupata vitanda na magodoro ili waondokane na adha hiyo ambayo wanadai inawatesa hasa kipindi hiki cha baridi kali wilayani humo.

Walitoa kilio hicho juzi walipokuwa wanapokea msaada wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kujenga bweni jipya shuleni hapo vilivyotolewa na Chama cha Maendeleo Makete (MDA). Chama hicho kimekuwa kikiwaunganisha wazaliwa wa Makete wanaoishi maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.

Mmoja wa wanafunzi hao, Judith Sanga, alisema bweni lao liliungua Juni, mwaka huu, na kuteketeza kila kitu kilichokuwamo ndani, hivyo wakawa hawana pa kulala wala vifaa vya kulalia hali iliyosababisha waondolewe shuleni kwa muda.

Alisema baada ya kurejea shuleni, bado hawana pa kulala, hivyo wanalazimika kulala madarasani ambako hata hivyo hakuna vitanda wala magodoro na hivyo wanalazimika kulala sakafuni.

"Vifaa vyetu vyote vya kulalia viliungua. Tunaiomba serikali na wadau wengine wa maendeleo watusaidie ili tupate angalau magodoro na mablanketi ya kulalia, kwa sasa huku kwetu kuna baridi kali sana hivyo kulala bila blanketi ni hatari," alisema.

Naye Anitha Mtweve aliiomba serikali iharakishe ujenzi wa bweni jipya ili waanze kulitumia tofauti na sasa ambapo wamegeuza baadhi ya madarasa kuwa mabweni hali ambayo inaweza ikasababisha tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa.

Akitoa taarifa ya tukio la moto uliounguza bweni hilo, Ofisa Elimu wa Kata ya Ikuwo, Asifiwe Malila, alisema baada ya bweni hilo kuteketea, Serikali ya Wilaya ya Makete ilitoa maelekezo ya kuwarejesha wanafunzi nyumbani kwa muda wa wiki moja.

Alisema maelekezo hayo yalikuwa na lengo la kuwapa nafasi wazazi kuwanunulia watoto wao vifaa vingine ikiwamo magodoro, mashuka na mablanketi na kwamba baada ya kurejea baadhi walishindwa kupata vifaa hivyo.

Alikiri baadhi ya wanafunzi kulala sakafuni kwenye madarasa kutokana na kukosa vifaa vya kulalia na kwamba kwa sasa wanaendelea na juhudi mbalimbali ili kuhakikisha wanafunzi wanapata mahali sahihi pa kulala.

Akikabidhi msaada wa vifaa hivyo vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni saba, Katibu wa MDA, Awadi Mpandila, alisema baada ya kupata taarifa za tukio hilo waliamua kuchangishana ili kuwasaidiwa wanafunzi wa shule hiyo.

Aliahidi chama hicho kuendelea kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo wilayani humo kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo.



## Rais Mwinyi akutana na mabalozi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekutana na kufanya mazungumzo na mabalozi mbalimbali wanaoziwakilisha nchi zao nchini Tanzania.

Rais Dk. Mwinyi awali alikutana na Balozi wa Kuwait nchini Tanzania, Mubarak Mohammed Alsehaijan.

Aliishukuru Serikali ya Kuwait kwa kuendeleza uhusiano wa kihistoria kati yake na Zanzibar pamoja na kuipatia Zanzibar misaada mbalimbali katika sekta za kijamii.

Katika hatua nyingine, Rais Dk. Mwinyi alikutana na Balozi wa Jamhuri ya Rwanda, Meja Jenerali Charles Karamba na katika mazungumzo hayo, Balozi Karamba alimweleza Rais mpango wa Shirika la Ndege la Rwanda 'Air Rwanda' kuanza safari zake kati ya Kigali na Zanzibar ifikapo katikati ya mwaka 2022, hatua ambayo itaimarisha sekta ya utalii kwa Zanzibar na Rwanda.

Balozi Karamba alimtaarifu Rais kuhusu mwaliko maalum waliouleta Zanzibar wa kuanzisha ushirikiano baina ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na Bodi ya Maendeleo Rwanda (RDB), unaolenga ushirikiano wa kiuwekezaji na kuwa na kituo kimoja cha kibiashara baina ya Zanzibar na Rwanda.

Wakati huo huo, Rais Dk. Mwinyi alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regina Hess, ambaye alifika Ikulu Zanzibar kuelezea mipango ya ushirikiano wa kimaendeleo kati ya Zanzibar na Ujerumani hususani kwenye eneo la uboreshaji wa huduma za maji na michezo.

Pia, alikutana na Mwakilishi wa Heshima wa Jamhuri ya Slovakia nchini Tanzania, Moustafa Khataw, ambaye alimtaarifu Rais mpango wa kuanza kwa safari za ndege za moja kwa moja kutoka Slovakia mpaka Zanzibar.

Kwa upande wake Rais Dk. Mwinyi alimtaka mwakilishi huyo kushajiisha wawekezaji wa Slovakia na kusisitiza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatilia mkazo dira ya uchumi wa bluu, ikiwamo uvuvi wa bahari kuu pamoja na mafuta na gesi huku akibainisha kuwapo rasilimali za kutosha baharini ambazo bado hazijatumika ipasavyo.

# Wataka kisiwa cha Mnemba kulindwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa imetoa ushauri kwa serikali kuhakikisha kisiwa cha Mnemba kinalindwa, kinaenziwa na kinaendelezwa licha ya kuwa serikali kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), kutoa utaratibu wa kukodishwa kwa visiwa vidogo vilivyomo Zanzibar.

Mwenyekiti wa Kamati ya kusimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa, Hassan Hafidh, aliyasema hayo jana walipofanya ziara ya kuangalia maeneo ya hifadhi za mazingira na kushuhudia uharibifu wa mazingira unaotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Hassan alisema watakaokodisha visiwa wawe watiifu katika kulinda na kuhifadhi mazingira ya visiwa na kuwasikiliza wataalamu ushauri wanaoutoa ili kuvilinda visiwa viendelee kuwapo.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo waliishauri serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kuhakikisha maeneo yaliyochimbwa mchanga yanarudi katika uhalisia wake kwa kuotesha miti ya asili ili kuepuka athari zaidi za kimazingira zinazoweza kutokea na kuhatarisha usalama wa maeneo jirani na wananchi.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omar Dadi Shajak, alisema kuna kazi kubwa ya kuhifadhi mazingira kwenye kisiwa cha Mnemba na vingine vyote vya Unguja na Pemba ili kukuza uchumi wa nchi.

Dk. Shajak alisema pamoja na kukuza uchumi wa nchi pia wananchi wanaozungukwa na kisiwa cha Mnemba waweze kunufaika na kuona umuhimu wa uhifadhi wa kisiwa ambacho ni moja kati ya rasilimali muhimu za Zanzibar.

"Ni lazima tuweke mazingira ambayo yanakuza uchumi wetu tusibakie tu kuwa tuna rasilimali halafu zimekaa tukaanza kuzivuruga Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inachukua nafasi yake katika kuhakikisha elimu inatolewa, mazingira yanahifadhiwa na sheria zinafuatwa katika kila hatua," alisema Dk. Shajak.

Mkurugenzi wa hoteli ya Kisiwa cha Mnemba, Jonathan Braack, alisema mmong'onyoko mkubwa wa fukwe hasa upande wa Mashariki na Kusini ya kisiwa hicho, uegeshaji na utupaji mbaya wa nanga za boti za kitalii ambao huharibu mwamba na idadi kubwa ya watalii wanaoogelea kwa wakati mmoja ndani ya mwamba wa hifadhi ni changamoto ambazo zinakikabili kisiwa hicho.

Jonathan alisema baadhi ya hatua zinazochukuliwa kutatua changamoto hizo ni kuhamasisha upandaji na utunzaji wa miti ya asili katika kisiwa cha Mnemba ili kurudisha uoto wa asili na kuimarisha uhimili wa kisiwa hicho kutoa elimu na kushirikiana na vijiji jirani katika kukiweka salama kisiwa cha Mnemba na kusaidia miradi kadhaa ya wanajamii.

Kisiwa cha Mnemba ni miongoni mwa visiwa vidogo ambacho kipo kilomita tatu kutoka usawa wa bahari na Kaskazini Mashariki mwa kisiwa cha Unguja chenye ukubwa wa hekta 10.74 ina vivutio vingi ikiwamo kivutio cha matumbawe ambayo yapo katika eneo la hifadhi ya bahari, kina sifa za kipekee ukilinganisha na visiwa vyengine ambapo asili yake imetokana na uwepo wa fungu mchanga linalozunguka kisiwa chote.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Abasi Juma Muhunzi (wapili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu mgogoro wa chama hicho unaoendelea sasa. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Vyombo vya ulinzi vyaagizwa kulinda karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), Komodoo Azan Msingiri, amevitaka vyombo vya ulinzi na usalama kisiwani Pemba kushirikiana katika kulinda zao la karafuu lisisafirishwe kwa njia ya magendo.

Alisema hayo jana Pemba, wakati akizungumza na Masheha wa shehia mbalimbali za mkoa huo.

Alisema yeye amechukua juhudi binafsi za kufika huko kwa lengo la kuisaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar isipoteze mapato yake kwa njia zisizo halali kisheria.

Alisema Masheha ndiyo watendaji wa kwanza katika ngazi ya serikali na wana uelewa mkubwa kwa wananchi wao ambao wanaishi nao katika shehia zao.

Aidha Komodoo Msingiri aliwashauri masheha kufuatilia kwa karibu zaidi wananchi wanaomiliki mikarafuu kuhakikisha karafuu wanazochuma wanaziuza serikalini.

Alieleza kuwa kumezuka tabia ya kuchukua vibali vya kuuzia karafuu, lakini wanaochukua vibali hivyo hawarejeshi risiti walizouza karafuu kwa sheha ili kutambua ukweli wa uuzwaji wa karafuu hizo katika sehemu husika iliyowekwa na serikali ambayo ni Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC).

Komodoo Msingiri, alisema mwananchi yeyote hana ruhusa ya kuweka karafuu ndani ya nyumba yake hata akiwa hajawa tayari kuuza kufanya hivyo ni kosa kisheria badala yake anatakiwa kuzihifadhi karafuu hizo katika Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC).

Hata Hivyo, aliwataka masheha kuwa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama kwa lengo la kutoa taarifa sahihi Ili zifanyiwe kazi kwa maslahi ya taifa.

Naye Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na wakuu wa wilaya kuunga mkono juhudi za mkuu huyo pamoja na kikosi cha KMKM katika udhibiti wa zao hilo lisisafirishwe kwa njia za magendo.

Alisema Komodoo Msingiri ni kiongozi mwenye msimamo na kutimiza ahadi kwasababu aliahidi kufunga kambi Pemba wakati wa karafuu utakapofika alipoenda kujitambulisha kwa mara ya kwanza baada ya kuapishwa kuwa Mkuu wa KMKM.

Salama alisema ni jambo la aibu kuonekana nchi ya Kenya inapata nafasi ya kwanza kwa kuzalisha karafuu wakati Zanzibar inasifika tokea asili kwa zao hilo.

Aidha, aliahidi kutimiza ahadi za ushirikiano ili kazi ziende vizuri kwasababu kikosi cha KMKM kimeonyesha nia ya dhati kwa kuleta boti zinazoenda kwa kasi katika kampeni hiyo ya udhibiti wa karafuu zisitoroshwe nje ya nchi.

Kwa upande wao masheha wa shehia mbalimbali walimwomba Mkuu wa KMKM Commodore Azana Msingiri, kudumisha doria katika maeneo yenye Bandari bubu ambazo ni nyingi kisiwani humo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU** KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTELEWA KWA VYETI (LEAVING CERTIFICATE)



**EMMANUEL ONESMO WILLIAM** anatangaza kupotelewa na Leaving certificate, ya kidato cha nne Bulima Sekondari Busega Simiyu Index namba **S0423-0069** ya Mwaka 2001 na Leaving Certificate ya Kidato cha Sita ya Taqwa Sekondari Mwanza Index namba **S0578-0599** ya mwaka 2005 kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichokaribu Polisi taarifa **MWA/NY/RB/411512/2021**

116426102

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya CHAMWINO MJINI**
**Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**
**Shauri la Ndoa Na. 45/2021**
**Jina la Mdai FLORA FELIX MANYAMA**
**Jina la mdaiwa MASINDOKI KENNEDY MASINDOKI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa MASINDOKI KENNEDY MASINDOKI**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**TALAKA NA MATUNZO YA MTOTO**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 03 mwezi 09 Mwaka 2021 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 26 mwezi 08 mwaka2021.

HAKIMU

116426202

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **SIMBA MTOTO TRANSPORT AND LIME SUPPLIES LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SCANIA yenye namba za usajili **T 153 DUX.** Yenye Engine namba **8289585** na Chassis namba **3900478.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **TAN/RB/415838/2021.**

116426002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**Ombi la CHARLES STANSLAUS MALLYA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu THOMAS STANSLAUS MALLYA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 23/8/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa

116425902

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BAJAJ BOXER** yenye namba za usajili MC 993 BVA,chasis namba **MD2A21BY7HWG87491** engine namba **PF2WHG77967,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DSM/PHQ/RB/561593/2021**

116426602

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAIKA RAYMOND KIRIA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX** yenye namba za usajili **T572 AEB** Kadi namba **7451691** Lenye chases namba **YN800002200** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/406999/2021**

116427002

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FOXES COMMUNITY AND WILDLIFE CONSERVATION** wanatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T770 DGB** Lenye chases namba **KZH201000059** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/412241/2021**

116427102

---

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa Kwa*
*Kutangaza*
*Nasi Kwa Bei Poa*

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Hichilema ‘agoma’ kuishi Ikulu

**Lusaka,** ZAMBIA

RAIS mpya wa Zambia Hakainde Hichilema, hatatoka kwenye makazi yake binafsi kwenda Ikulu, ripoti za gazeti la serikali la Zambia, Daily Mail, zimeeleza.

Hatua hiyo imeelezwa pamoja na kwamba mtangulizi wake Edgar Lungu, anatoka kwenye makazi ya Ikulu wiki hii.

Katibu Mkuu wa chama cha Hichilema, Batuke Imenda, amenukuliwa akisema kuwa kiongozi huyo mpya atafanya kazi ikulu, lakini ataendelea kuishi kwenye makazi yake binafsi, yaitwayo nyumba ya jamii.

"Kama alivyosema kabla ya kula kiapo, rais wetu ataendelea kuishi kwenye nyumba yake huko New Kasama. Anajisikia vyema akiwa kwenye nyumba ya jamii. Unapolinganisha maeneo hayo mawili, nyumbani kwake ni bora," Imenda alisema kwa mujibu wa Zambia Daily Mail.

Tangazo la Hichilema kwamba hataenda kuishi ikulu limekuja baada ya Lungu, ambaye aliangushwa kwa zaidi ya kura milioni moja kwenye uchaguzi Agosti 12, mwaka huu, kuchapisha ujumbe kwenye ukurasa wa twitter akisema amekuwa na kumbukumbu nzuri ya muda alioutumia ikulu.

**BBC**



Askari wa Kikosi cha Usalama Mpakani (BSF) akiruka moto, kuonyesha umahiri wake wa kuendesha pikipiki wakati wa onyesho barabarani, kwenye maadhimisho ya miaka 75 ya Uhuru wa India, jijini Ahmedabad, nchini India. **PICHA: REUTERS**

## Utafiti: Malaria kupunguzwa kwa asilimia 70

**Ouagadougou,** MALI

UTAFITI uliofanywa Afrika Magharibi, unaashiria kuchanganya chanjo ya malaria na dawa ya kuzuia ugonjwa huo, kunaweza kupunguza visa vya watu kulazwa hospitali au kufariki kwa zaidi ya asilimia 70.

Lakini mchanganyiko huo wa dawa unastahili kutumiwa kabla ya msimu wa mvua.

Malaria huathiri zaidi watoto na vijana, ukiua zaidi ya watu 400,000 kila mwaka hususan barani Afrika.

Utafiti huo mpya ulioshirikisha watoto 6,000, walio na kati ya miezi mitano na 17 nchini Burkina Faso na Mali, ambazo zimeathiriwa sana na magonjwa yanayosababishwa na mbu.

Wanasayansi katika London School of Hygiene & Tropical Medicine, ambao walisaidia kufanya utafiti huo, wameelezea matokeo hayo kama ya kushangaza.

Wanatarajia mbinu hiyo ya kuchanganya dawa itasaidia kuzuia malaria katika sehemu nyingi za Afrika.

**BBC**

## Japan yasitisha chanjo dozi milioni moja za Moderna

**Tokyo,** JAPAN

JAPAN itasitisha utoaji wa dozi milioni 1.63 za chanjo ya Moderna, dhidi ya virusi vya corona, baada ya ripoti kuibuka kuhusu uchafuzi au sibiko kwenye chupa ndogo kadhaa za chanjo hiyo.

Kampuni ya kutengeneza chanjo Takeda pamoja na wizara ya Afya zimesema hayo jana.

Takeda ambayo ndiyo kampuni inayohusika na uuzaji pamoja na usambazaji wa chanjo ya Moderna nchini Japan, ilisema imepokea ripoti za uchafu kupatikana ndani ya chupa za chanjo, ambazo hazijafunguliwa.

Takeda haikutoa maelezo zaidi kuhusu aina ya uchafu uliopatikana, ilisema haijapokea ripoti yoyote ya kusababisha wasiwasi wa kiafya kutokana na dozi zilizoathiriwa.

Kampuni hiyo imeongeza kuwa baada ya kushauriana na wizara ya Afya, wameamua kusitisha matumizi ya dozi hizo kuanzia jana.

Na kwamba tayari imeshaiarifu kampuni ya Moderna na kutaka uchunguzi wa haraka ufanywe.

Kampuni ya Moderna hata hivyo haikutoa jibu la moja kwa moja kuhusu ombi hilo.

**DW**

## Onyo latolewa kitisho ugaidi uwanja Kabul

**Kabul,** AFGHANISTAN

MATAIFA mbalimbali ya kigeni yanahofia huenda kukatokea shambulizi la kigaidi kwenye uwanja wa ndege wa Kabul, Afghanstan.

Nchi za Australia, Marekani na Uingereza zimetoa tahadhari hiyo kwa raia wake, ambao bado wapo nchini humo na kuwataka kuondoka haraka kwenye uwanja wa ndege.

Jana asubuhi, maofisa wa Taliban, waliahidi kutoa usalama nje ya uwanja wa ndege wa Kabul, ripoti za idara za ujasusi zinazoelezea tishio kubwa kutoka kwa wapiganaji wa IS, haziwezi kupuuzwa, alisema mwanadiplomasia mmoja kutoka nchi wanachama wa NATO katika mji mkuu wa Afghanistan.

Watu zaidi ya 82,000 wameondolewa jijini Kabul, wakati huu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani akieleza idadi ya Wamarekani ambao wamesalia nchini humo.

**RFI**

## Shirika la ndege la Afrika Kusini kuanza tena safari

**Johannesburg, AFRIKA KUSINI**

SHIRIKA la ndege la Afrika Kusini, ambalo siku za hivi karibuni lilibinafsishwa katika juhudi za kuliokoa lisifilisike, limesema litaanzisha tena safari zake mwezi Septemba.

Shirika hilo ambalo lilikuwa la pili kwa ukubwa barani Afrika, likitanguliwa na shirika la ndege la Ethiopia, lilinusurika kwa miaka mingi kutokana na ruzuku za serikali na lilisitisha safari zake hata kabla ya janga la COVID 19.

"Chini ya mwezi mmoja, ndege za shirika hilo zitaanza tena kuonekana kwa mujibu wa taarifa kutoka shirika hilo.

Awali, shirika hilo lilisema kuwa safari za ndani kutoka Johannesburg kuelekea Cape Town, pamoja na safari kwenye miji mingine ya Afrika kama Accra, Kinshasa, Harare, Lusaka na Maputo zitaanza karibuni.

**VOA**

## Rais wa zamani Chad Habre azikwa uhamishoni

**N' Djamena,** CHAD

SIKU mbili baada ya kifo cha Rais wa zamani wa Chad Hissène Habré, kutokana na ugonjwa wa COVID-19, amezikwa jana, nchini Senegal.

Uamuzi huo ulikuwa ukisubiriwa wakati suala la kurejeshwa kwa mwili wake kuja Chad lilipoibuka.

Kiongozi huyo wa zamani wa Chad, alikuwa akiishi Senegal kwa miaka 31, baada ya kuondolewa mamlakani na Idriss Deby.

Alihukumiwa kifungo cha maisha mwaka 2016 kwa uhalifu dhidi ya binadamu wakati wa utawala wake kuanzia mwaka 1982 hadi 1990.

Mwili wa Hissène Habré ulipelekwa katika msikiti wa Omar huko Dakar na mazishi kufanyika katika makaburi ya Waislamu ya Yoff katika mji mkuu wa Senegal.

Kulikuwa na mvutano kati ya wake wawili wa Hissene Habre, kuhusu wapi atazikwa mume wao, lakini pande zote mbili ziliafikiana na kuamua azikwe nchini Senegal.

Kwa sababu jioni siku alipofariki, Fatimé Raymonne Habré, mmoja wa wake zake, alitangaza kwamba anataka mumewe azikwe kwa muda Senegal.Alikimbilia uhamishoni nchini Senegal baada ya kuhukumiwa kifo akiwa hayupo nchini mwake.

**BBC**

MECHI KALI

HOME

AL AHLY CAIRO

1.19 | 7.12 | 10.88

ASWAN

AWAY

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND


SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 450

# ARTETA ASIFIA KIWANGO ARSENAL IKIPIGA MTU 6



**LONDON, England**

MIKEL Arteta amesifia ari iliyoonyeshwa na kikosi chake cha Arsenal licha ya kuanza vibaya msimu mpya wa Ligi Kuu kwa kupoteza mechi mbili mfululizo, baada ya kupata ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya West Brom kwenye mchezo wa Kombe la EFL, juzi.

Arsenal hadi sasa hawana pointi kwenye Ligi Kuu England licha ya kucheza mechi mbili na pia hawana bao hata moja.

Lakini Jumatano waliamka na kuwafumua West Brom mabao 6-0 kwenye mchezo wa EFL, huku nahodha wake, Pierre-Emerick Aubameyang akifupiga matatu 'hat-trick'.

Aubameyang pia alitengeneza bao kwa Nicolas Pepe, ambaye naye alitoa asisti kwa Alexandre Lacazette, huku pia Bukayo Saka akifunga.

Ulikuwa ushindi wa kwanza mkubwa zaidi katika maisha ya ukocha ya Arteta, huku Arsenal awali ikiwa haijafunga mabao sita tangu mwaka 2017.

Alipoulizwa na Sky Sports kuhusu kiwango cha timu yake ambayo sasa itacheza na AFC Wimbledon katika raundi ya tatu, Arteta alijibu: "Ari ilikuwa kubwa kwa timu, tangu dakika ya kwanza walionyesha kwamba, wana njaa na kitu fulani.

"Hilo kwa hakika limeifanya timu kuamka kutoka kwenye wakati mgumu wa mwanzo wa Ligi Kuu, nina imani ari hii itaendelea kwa mechi zetu zinazokuja

"Wachezaji walijua kwamba, wanaingia kwenye mchezo huo wakiwa wametoka kupata matokeo mabaya zaidi kwenye Ligi Kuu, hivyo walikuwa na kila sababu ya kuhakikisha wanashinda mchezo huo."

# *Kane kubakia Spurs msimu huu*

**LONDON, England**



HARRY Kane amesema kuwa kwa sasa hataondoka ndani ya kikosi cha Tottenham Hotspur na atabaki kwa msimu mzima baada ya dili lake la kuibukia Manchester City kushindikana.

Kane amebakiza mkataba wa miaka mitatu kuendelea kuitumia Spurs na aliomba kuondoka kwenye kikosi hicho msimu huu ili aweze kutafuta changamoto mpya.

Lakini amekwama baada ya mazungumzo ya muda mrefu ambayo yalikuwa yakifanyika dhidi ya Man City kushindikana.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Kane ambaye ni nahodha wa timu ya Taifa ya England, aliandika kuwa anafurahi kubaki hapo na atatumia nguvu zake nyingi katika kuipa mafanikio timu hiyo kwa kushirikiana na wachezaji wenzake.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nuno Espirito Santo, amesema hiyo ni habari njema na kubwa kwa kila mtu kwa kuwa Kane ameamua kubaki katika kikosi hicho na ana matumaini watafanya vizuri katika mashindano ambayo watashiriki.

"Ni habari kubwa kwa kila mtu kusikia kwamba Kane anabaki, tutafanya vizuri na tutafanya naye kazi leo tukiwa na uhakika wa uwapo wake kesho, hilo limeisha."

HABARI MICHEZO

,150,500

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/08/21 | 17:00 | Brighton vs Everton | 2.31 | 3.27 | 3.16 |
| 02. 28/08/21 | 17:00 | Newcastle vs Southampton | 2.60 | 3.40 | 2.65 |
| 03. 28/08/21 | 17:00 | Huddersfield vs Reading | 2.42 | 3.20 | 2.86 |
| 04. 28/08/21 | 17:00 | Preston vs Swansea | 2.46 | 3.26 | 2.77 |
| 05. 28/08/21 | 17:00 | Luton Town vs Sheffield Utd | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 06. 28/08/21 | 18:00 | Celta Vigo vs Athletic Bilbao | 2.42 | 3.22 | 3.02 |
| 07. 28/08/21 | 19:30 | Liverpool vs Chelsea | 2.45 | 3.36 | 2.86 |
| 08. 28/08/21 | 20:30 | Real Oviedo vs Tenerife | 2.60 | 2.85 | 2.95 |
| 09. 29/08/21 | 16:00 | Burnley vs Leeds | 3.11 | 3.41 | 2.27 |
| 10. 29/08/21 | 16:00 | Angers vs Rennes | 2.85 | 3.20 | 2.50 |
| 11. 29/08/21 | 16:30 | Union Berlin vs Monchengladbach | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 12. 29/08/21 | 20:30 | Cadiz CF vs Osasuna | 3.01 | 3.01 | 2.56 |
| 13. 29/08/21 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Granada | 2.61 | 3.22 | 2.77 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 27 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:30 | 5741 | Ural Yekaterinburg vs Rostov | 3.35 | 3.11 | 2.20 |
| 18:30 | 4054 | Viljandi Tulevik vs Tammeka Tartu | 2.12 | 3.67 | 2.85 |
| 18:30 | 4484 | FK Khimki vs Nizhny Novgorod | 2.08 | 3.24 | 3.49 |
| 18:30 | 5154 | Japs vs Kapa | 1.42 | 5.20 | 6.20 |
| 19:00 | 2489 | Backa Topola vs Mladost Lucani | 1.39 | 4.45 | 6.58 |
| 19:00 | 2959 | Dinamo Moscow vs Lokomotiv Moscow | 2.15 | 3.41 | 3.16 |
| 19:00 | 5460 | Pisa vs Alessandria | 2.30 | 2.92 | 3.36 |
| 19:30 | 2237 | Chernomorets Odessa vs Oleksandria | 3.24 | 3.24 | 2.09 |
| 19:30 | 4834 | Udinese vs Venezia | 1.69 | 3.81 | 5.02 |
| 19:30 | 5165 | SV Lafnitz vs SV Horn | 1.75 | 3.78 | 3.88 |
| 19:30 | 5693 | FC Juniors OO vs Blau Weiss Linz | 3.62 | 3.77 | 1.81 |
| 20:00 | 1183 | Aalborg vs Nordsjalland | 2.02 | 3.45 | 3.45 |
| 20:00 | 1725 | SC Schwaz vs SV Fugen | 1.12 | 7.94 | 12.60 |
| 20:00 | 2019 | Creteil vs Chateauroux | 3.91 | 2.93 | 2.05 |
| 20:00 | 3573 | Villefranche Sur Saone vs Concarneau | 2.23 | 2.79 | 3.58 |
| 20:00 | 4795 | Ceramica Cleopatra vs Ismaily SC | 2.51 | 3.00 | 2.91 |
| 20:30 | 1833 | FC Krasnodar vs Rubin Kazan | 1.67 | 3.85 | 4.64 |
| 20:30 | 3548 | Antalyaspor vs Caykur Rizespor | 2.17 | 3.31 | 3.21 |
| 21:00 | 1444 | Fortuna Sittard vs Waalwick | 1.96 | 3.59 | 3.49 |
| 21:00 | 3591 | Jong Utrecht vs Telstar | 2.48 | 3.60 | 2.48 |
| 21:00 | 4856 | Mallorca vs Espanyol | 2.67 | 2.97 | 2.92 |
| 21:00 | 5001 | FC Eindhoven vs Den Bosch | 2.00 | 3.65 | 3.22 |
| 21:00 | 5371 | Belenenses vs Moreirense | 3.05 | 2.95 | 2.45 |
| 21:00 | 5566 | FK Pohronie vs Dunajska Streda | 4.27 | 3.73 | 1.69 |
| 21:15 | 3252 | NK Celje vs NK Radomlje | 1.75 | 3.58 | 4.07 |
| 21:25 | 2859 | Liebherr Gak vs Vorwarts Steyr | 1.41 | 4.67 | 5.83 |
| 21:30 | 1136 | Borussia Dortmund vs Hoffenheim | 1.44 | 5.15 | 5.74 |
| 21:30 | 1429 | FC Aarau vs FC Vaduz | 1.96 | 3.67 | 3.19 |
| 21:30 | 1949 | Stomil Olsztyn vs LKS Lodz Pss | 4.16 | 3.48 | 1.76 |
| 21:45 | 1076 | Newry City AFC vs Ards FC | 2.27 | 3.58 | 2.66 |
| 21:45 | 1286 | Burton vs Cheltenham | 2.22 | 3.15 | 3.25 |
| 21:45 | 1293 | Edinburgh City vs Elgin City | 2.28 | 3.33 | 2.80 |
| 21:45 | 1704 | Verona vs Inter | 5.21 | 4.31 | 1.58 |
| 21:45 | 2655 | Portadown FC vs Glenavon | 4.34 | 4.15 | 1.60 |
| 21:45 | 2689 | Caernarfon Town vs Newtown AFC | 2.80 | 3.75 | 2.28 |
| 21:45 | 3580 | Dundalk FC vs St Mochtas FC | 1.13 | 7.19 | 14.57 |
| 21:45 | 4177 | UCD Dublin vs Longford Town | 2.30 | 3.38 | 2.75 |
| 21:45 | 4238 | Rochdale vs Colchester | 2.06 | 3.34 | 3.39 |
| 21:45 | 4728 | Cork City vs St Patricks | 6.59 | 4.07 | 1.43 |
| 21:45 | 4837 | Waterford Utd vs Kilnamanagh AFC | 1.13 | 7.17 | 13.57 |
| 21:45 | 5185 | Larne vs Coleraine FC | 2.04 | 3.48 | 3.14 |
| 21:45 | 5220 | Adana Demirspor vs Konyaspor | 2.07 | 3.35 | 3.40 |
| 22:00 | 1228 | National Bank vs Zamalek | 5.30 | 3.29 | 1.72 |
| 22:00 | 3766 | Nantes vs Lyon | 4.27 | 3.87 | 1.75 |
| 22:00 | 4994 | Al Ahly Cairo vs Aswan | 1.19 | 7.12 | 10.88 |
| 22:00 | 5193 | Finn Harps vs Derry City | 3.53 | 3.24 | 1.99 |
| 23:00 | 1518 | Malaga vs Alcorcon | 2.40 | 2.81 | 3.31 |
| 23:15 | 1532 | Valencia vs Alaves | 1.85 | 3.47 | 4.42 |
| 23:15 | 3279 | GD Estoril vs Maritimo | 2.20 | 3.11 | 3.35 |
| 23:30 | 3579 | Real Garcilaso vs Club Cienciano | 2.92 | 3.06 | 2.35 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# INSIGNE AWINDWA LIVERPOOL



**LIVERPOOL, England**

NAHODHA wa Napoli, Lorenzo Insigne anawindwa na klabu za Ligi Kuu England, Liverpool na wapinzani wao wa jiji moja, Everton.

Isigne alifanya vizuri kwenye michuano ya Euro 2020 wakati alipoisaidia timu yake ya Taifa ya Italia kutwaa ubingwa huo.

Mbali na timu hizo, pia Inter Milan ambayo inayoshiriki Ligi Kuu Italia, Serie A, inaipigia hesabu saini ya nyota huyo ambaye ana umri wa miaka 30.

Raia huyo wa Italia ni moja ya nyota ambao wamekuwa wakitajwa sana kusepa ndani ya timu yake ya sasa inayoshiriki Serie A, hivyo huenda atakuwa kwenye changamoto mpya dili lake likijibu.

Kwa upande wa Liverpool wao imeelezwa kuwa wanahitaji saini za wachezaji watatu kabla ya dirisha kufungwa.

Na miongoni mwa nyota wanaotajwa ni pamoja na Insigne ingawa pia Inter Milan wao wanasubiri dili lao kujibu kwa mshambuliaji huyo ambaye ni chaguo lao pia.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot SportPesa, Selemani Mbonde, akionyesha mfano wa hundi ya shilingi milioni 5.7 za Tanzania baada ya kushinda, kubashiri kwa usahihi mechi 11 kati ya 13 za Jackpot. Wiki hii Jackpot ya SportPesa ni shilingi 260,453,360. **PICHA: SPORTPESA**

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YATAJIWA BEI YA KUMNASA MBAPPE

●●● Ilikuwa tayari kutoa euro milioni 160, lakini sasa dau lake limetajwa ni euro milioni 220...

**PARIS, UFARANSA**

KLABU ya Paris Saint-Germain inataka kiasi cha euro milioni 220 ili kuamwachia mchezaji anayataka kuondoka na anayewaniwa na Real Madrid, Kylian Mbappe, kwa mujibu wa ukurasa wa kwanza wa gazeti la Diario AS la jana, Alhamisi.

Imethibitishwa kwamba, Mbappe anataka kuondoka Paris Saint-Germain, licha ya ujio wa mkali, Lionel Messi klabuni hapo.

Madrid sasa wanatakiwa wafikie makubaliano na PSG kama wanataka kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto kabla ya dirisha lake kufungwa, au wasubiri hadi msimu ujao wamchukue akiwa huru.

Madrid iliripotiwa kwamba, inataka kutoa ofa ya kiasi cha euro milioni 160 kwa Mbappe, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu wa 2021-22.

Mapema Jumatano, Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Leonardo alithibitisha kwamba Mfaransa huyo yupo tayari kuondoka hapo jijini Paris.

Na sasa PSG imetaja bei rasmi ya nyota wake huyo mshindi wa Kombe la Dunia, huku tovuti ya RMC ikidai kwamba, Madrid itaongeza ofa yake kwa ajili ya Mbappe.

Miamba wa Ligi Kuu England, Liverpool na Manchester United pia wamekuwa wakihusishwa na nia ya kuwania kumsajili nyota huyo.

## ZISIKUPITE

### MAN CITY NA RONALDO
MANCHESTER City wanaweza kumgeukia mshambuliaji wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, baada ya nahodha huyo wa England, Harry Kane kusema anabaki Tottenham Hotspur. ***(ESPN)***

### KANE ALIA NA LEVY SPURS
HARRY Kane mwenye umri wa miaka 28, amesikitishwa na Mwenyekiti wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy kutomruhusu aondoke na anaweza akasaini mkataba mpya. ***(Telegraph)***

### GUARDIOLA KUGEUKIA TAIFA
KOCHA wa Pep Guardiola, ataondoka Manchester City pale mkataba wake utakapomalizika msimu wa mwaka 2022-23 ili kupumzika kabla ya kuhamia kufundisha timu za taifa. ***(Globo, via Manchester Evening News)***

### CONTE AHUSISHWA NA ARSENAL
KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte anahusishwa na mipango ya kuchukua nafasi ya Mikel Arteta kule Arsenal. ***(Independent)***

### MOURINHO KWA LOFTUS-CHEEK
KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, amepanga kutumia pauni milioni 13.5 kwa ajili ya kiungo wa Chelsea, Ruben Loftus-Cheek mwenye umri wa miaka 25. Nyota huyo aliwahi kidogo kufanya kazi na Mourinho wakati Mreno huyo aliporejea kuifundisha Chelsea kwa mara ya pili. ***(Mail)***

### UNITED, CAMAVINGA HAKIELEWEKI
MANCHESTER United haitaweza kupeleka dau kwa ajili ya kiungo wa Rennes, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 18, au kiungo wa Atletico Madrid na Hispania, Saul Niguez mwenye miaka 26, kama haitauza wachezaji wake kupata fedha za kuingia sokoni. ***(ESPN)***

### ARTETA HATAFUKUZWA ARSENAL
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta hayuko katika hatari ya kutimuliwa kibarua chake licha ya 'Washikabunduki hao kuanza vibaya msimu huu wa Ligi Kuu England. ***(Mail)***

### CHELSEA SAFI KWA NIGUEZ
CHELSEA wanaelezwa wako katika nafasi nzuri ya kumsajili, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 26, huku Atletico Madrid wakiwa tayari kumuuza raia huyo wa Hispania. ***(Express)***

### SEVILLE IMEIGOMEA CHELSEA
KLABU ya Sevilla imesema kwamba, walikataa ofa ya Chelsea kwa ajili ya kumsajili mlinzi wake, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22 na hawahitaji kuuza wachezaji. ***(Goal)***

### MORIBA NI CHELSEA AU LEIPZIG
KIUNGO wa Barcelona, Ilaix Moriba huenda akatua Chelsea ama RB Leipzig kama kinda huyo mwenye umri wa miaka 18 raia wa Guinea hataongeza mkataba mpya na wakali hao wa LaLiga. ***(Mundo Deportivo)***

### WILLIAN SAFI CORINTHIANS
WINGA wa Arsenal na Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 33, wakati wowote atakamilisha uhamisho wake wa kutua klabu ya Corinthians. ***(Sun)***

# JEMBE ULAYA AKUNWA WAKONGO KIKOSI YANGA

**Na Donald Lukele, TUDARCo**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, akisema anahitaji kipindi cha miezi angalau mitatu ili kupata muunganiko mzuri wa kikosi chake, mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Bakari Malima 'Jembe Ulaya', amewatoa hofu mashabiki wa klabu hiyo.

Baada ya kikosi cha Yanga kurejea nchini kikitokea kambini jijini Marrakesh, Morocco kilikokuwa kikijifua kujiandaa na msimu mpya, Nabi alisema bado hajapata muunganiko wa kikosi chake na atahitaji muda zaidi ili kuwaunganisha wachezaji ambao wengi ni wapya.

Hata hivyo, Jembe Ulaya akizungumza na mwandishi wetu katika mahojiano maalum kuhusu matarajio yake katika kikosi hicho kuelekea msimu mpya wa 2021/22, kwanza aliisifu Kamati ya Usajili ya Yanga kwa kufanya usajili makini.

Kuhusu kauli ya kocha kuwa kikosi chake kitachelewa kupata muunganiko, Jembe Ulaya alisema hana shaka katika hilo kwa kuwa wachezaji wengi waliosajiliwa na timu hiyo msimu huu wanafahamiana na kutokana na kutoka nchi moja.

"Msimu ujao Yanga itafanya makubwa sana kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabigwa Afrika kwa kuwa wachezaji waliosajiliwa wana uzoefu wa michuano ya kimataifa, kamati ya usajili imezingatia kwa kusajili wachezaji wengi kutoka nchi moja (DR Congo), ili kuleta muunganiko wa haraka kutokana na kuelewana hata kwa lugha," alisema Malima

Aidha, Malima ambaye aliwahi kupata mafanikio makubwa ndani ya klabu hiyo wakati akiichezea miamba hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, alieleza kufurahishwa na usajili uliofanywa na klabu hiyo kuelekea msimu mpya kwa kuwa umezingatia ubora na uzoefu wa wachezaji kwenye michuano mikubwa Afrika.

Alisema viongozi wa Yanga wanapaswa kumpa muda wa kutosha ili kuweza kuimarisha kikosi chake kwa kuwa tayari ameonyesha mabadiliko husuan kuimarisha nidhamu ya wachezaji na katika benchi la ufundi.

"Nawaomba viongozi wa Yanga kumpa muda wa kutosha Nabi ili aijenge timu, ameonyesha juhudi kubwa kwa kujenga nidhamu ya wachezaji na hata benchi la ufundi, akipewa muda wa kutosha atafanya makubwa," alisema Jembe Ulaya

Kadhalika, Malima alieleza kufurahishwa kumwona aliyekuwa Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, akihamia rasmi Yanga, jambo ambalo alisema atasaidia kufanya makubwa katika klabu hiyo kama alivyokuwa akifanya kwa Wekundu wa Msimbazi hao, endapo akipewa ushirikiano wa kutosha.

Yanga msimu huu imesajili jumla ya wachezaji wanne kutoka DR Congo hivyo kufanya jumla kuwa watano pamoja na Mukoko Tonombe aliyesajiliwa msimu uliopita.




Beki wa kulia wa Azam FC, Nicolous Wadada (kushoto), akiwania kumiliki mpira dhidi ya mshambuliaji wa Red Arrows kwenye mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Levy Mwanawasa, Ndola nchini Zambia na wenyeji hao kuibuka na ushindi wa mabao 4-0. **PICHA: AZAM**

## Mtibwa yajisubirisha kwa Ame, Ndemla

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikitangaza rasmi kuwatoa kwa mkopo wachezaji wake, Said Ndemla na Ibrahim Ame, klabu ya Mtibwa Sugar imesema haijamalizana na klabu hiyo kwa asilimia zote, kwani kuna vitu ambavyo wanatakiwa kuvikamilisha.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mtibwa Sugar, Sabri Aboubakar, alisema ni kweli wapo kwenye mazungumzo na klabu ya Simba, lakini bado suala hilo halijakamilika.

"Ni kweli tumeongea nao kuhusu wachezaji hao, lakini bado dili halijakamilika kwa sababu kuna vitu ambavyo tunatakiwa tukamilishe ili liishe. Kwa hiyo subirini tu hivi karibuni, wao na wachezaji wengine ambao tutawasajili tutatoa tamko," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu huyo.

Awali, Kaimu Ofisa Habari wa klabu ya Simba, Ezekiel Kamwaga alisema kuwa wamewapeleka wachezaji wao kwa mkopo baada ya makubaliano na klabu hiyo.

"Ninavyokwambia ni kwamba tuna wachezaji watatu ambao tunawapeleka kwa mkopo kwenye timu tofauti, Ndemla anakwenda Mtibwa, Ame anakwenda Mtibwa na Kameta 'Duchu' anakwenda Biashara United," alisema Kamwaga.

Wakati Ndemla akiwa ni zao la kikosi cha pili cha Simba, Ame alisajiliwa na klabu hiyo msimu uliopita akitokea Coastal Union, huku Duchu akisajiliwa kutoka Lipuli FC.

Kwa sasa klabu nyingi ziko kwenye hekaheka za usajili kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakati huu dirisha la usajili likitarajiwa kufungwa Agosti 31, mwaka huu.

## Serikali yazitangazia neema klabu Ligi Kuu

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, imesema ipo mbioni kuanzisha sheria itakayolinda mali za klabu za soka ili kupambana na wanyonyaji.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Michezo wa wizara hiyo, Yusuph Singo, ambapo alisema muda umefika kwa klabu kunufaika kwa nembo zao.

"Wapo wafanyabiashara wachuuzi ambao wananufaika na mali za klabu hususan klabu kubwa, serikali imeliona hilo na sasa ipo mbioni kutunga sheria ambayo itawabana wanyonyaji na kuzifanya klabu kunufaika," alisema Singo.

Alisema klabu zinaingia gharama kutengeneza jezi na kuziagiza kutoka nje, lakini wapo wajanja wanaoghushi na kujiingizia mapato, hivyo serikali imedhamiria kukomesha unyonyaji huo.

"Niziambie klabu, serikali inathamini sana kile mnachokifanya katika kuendeleza michezo na kutengeneza ajira kwa vijana, sheria hii inayokuja itakuwa msaada mkubwa kwenu kuwatokomeza wanyonyaji hawa," aliongezea kusema Singo.

Mkurugenzi huyo alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya uzinduzi wa jezi mpya za Yanga uliofanyika juzi kwenye Mlimani City , Dar es Salaam akimuwakilisha mgeni rasmi, Waziri wa wizara hiyo, Innocent Bashungwa.

## Kamati ya Amani, wanahabari kukipiga

**Na Saada Akida**

KAMATI ya Amani ya viongozi wa dini mbalimbali wameandaa mechi ya kirafiki dhidi ya wanahabari za michezo, itakayopigwa Septemba Mosi, mwaka huu katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Sheikh Alhad Mussa Salum, ambaye ni mwenyekiti wa kamati hiyo, alisema lengo kubwa la kuandaa mechi hiyo ni kuiunga mkono serikali katika suala zima la usalama wa chanjo na kuipa jina la 'Mama Amechanja, Nasi Tukachanje'.

Alisema mechi hiyo itakuwa maalum kwa kuwaondoa hofu wananchi kuhusu usalama wa chanjo ya COVID-19.

"Hii mechi itakuwa ni kuhimiza Watanzania kwenda kupata chanjo ambayo ni salama na kufuata maelekezo ya Wizara ya Afya katika kuchukuwa tahadhari za kujinga na COVID-19,"alisema

Alisema waamuzi wa mechi hiyo ni Kamanda mstaafu, Suleiman Kova, akisaidiwa na Kamanda Kanda Maalum, Jumanne Muliro na Azim Dewji, huku makamisaa wakiwa IGP Simon Sirro na Mufti Sheikh Abubakar Zuber.

# Michezo

Ijumaa Agosti 27, 2021

Nipashe


HABARI UK.22



## Madrid yatajiwa bei ya kumnasa Mbappe

VISIKI...



Mabeki visiki wa kati wa Simba, Henoc Inonga Baka 'Varane', akiucheza mpira kwa kichwa huku Pascal Wawa akiruka kutaka kuucheza kwa mguu, wakati wa mazoezi ya timu hiyo iliyoweka kambi nchini Morocco kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Bara na michuano ya kimataifa. **PICHA: SIMBA**.

# SIMBA SASA KAMBI MAREKANI

## ●●● Kukipiga na klabu kubwa za MLS, kurejea Jumamosi ikitokea Morocco baada ya...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kikosi cha Simba kikitarajiwa kurejea nchini mwishoni mwa wiki hii kikitokea nchini Morocco, maandalizi ya msimu ujao wa 2022/23, kitakwenda kuweka kambi nchini Marekani kwa mwaliko ya Klabu ya D.C. United yenye makazi yake jijini Washington D.C.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba na mwekezaji wa klabu hiyo, Mohammed 'Mo' Dewji, ambaye kwa sasa yupo Marekani, amesema timu hiyo imeingia ushirikiano na Klabu ya D.C. United, ambayo imeipa mwaliko huo

Mo Dewji amesema mwaliko huo ameupata baada ya kukutana na mmoja wa wamiliki wa D.C. United, Jason Levien, anayeimiliki kwa pamoja na Erick Thohir tangu mwaka 2012 walipoinunua.

"Ilikua ni furaha kukutana na Jason Levien, ambaye ni mmiliki wa klabu ya mpira wa miguu ya D.C. United ambayo ina thamani ya dola za Kimarekani millioni 700.

"Nina furaha kutangaza ushirikiano mpya kati ya Klabu za D.C. United na Simba. Ifikapo mwaka 2022, Klabu ya Simba itasafiri kwenda Marekani kwa ajili ya mazoezi na maandalizi ya msimu mpya, na pia itashiriki katika mashindano ya kimataifa yatakayoandaliwa na Klabu ya D.C. United, ambayo yatahusisha timu za Ligi ya MLS (Ligi Kuu ya Marekani) na klabu za kutoka Amerika ya Kusini," alisema Dewji.

Katika hatua nyingine Kaimu Ofisa Habari wa Simba, Ezekiel Kamwaga, amesema kikosi cha Simba kitarejea nchini mwishoni mwa wiki, kilipoweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya na kisha Jumatatu ya Agosti 30, mwaka huu, kitaingia tena kambini nje ya Dar es Salaam, kuendelea na maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

> **Alisema baada ya kurejea wachezaji watapewa mapumziko ya siku mbili na kisha kurejea tayari kwa kwenda kuingia kambini sehemu nyingine.**

"Baada ya mechi yetu ya leo (jana), Jumamosi timu itarejea Tanzania na wachezaji watapewa mapumziko ya siku mbili baada ya hapo tutakwenda sehemu nyingine ambayo itajulikana siku hiyo kuendelea na Pre-Season yetu (maandalizi ya msimu mpya)," alisema Kamwaga.

Alisema msimu huu wamejipanga vizuri kuhakikisha timu inapata maandalizi mazuri na kuiendesha kisasa zaidi kwa kuzindua 'Simba SC APP', ambayo mashabiki, wanachama na yeyote anaweza kupata taarifa za uhakika kupitia mtandao huo.

"Simba sasa inakimbia, tumetoka kwenye mambo ya zamani na sasa kila mtu anaweza kupata taarifa za Simba kwa muda sahihi kupitia mtandao huo ambao utaghalimu Sh. 2,000 kwa mwezi, hii itasaidia klabu kupata mapato yake kupitia kwa wanachama," alisema Kamwaga.

Alisema kupitia mtandao huo, itawafanya mashabiki wa klabu hiyo waliokuwa nje ya nchini pamoja na waliopo mbali na timu, kupata fursa ya kuona timu yao na kupata taarifa kwa uharaka na uhakika.

Simba ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA, watashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa Septemba 25, mwaka huu kuvaana na watani zao, Yanga kwenye mechi ya Ngao ya Jamii, ambayo ni maalum kwa ajili ya ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu 2021/22 itakayoanza siku nne baada ya ufunguzi huo.

# Yanga yatoa neno kesi Morrison CAS

**Saada Akida na Faustine Feliciane**

HUKU mashabiki na wanachama wa Yanga shauku ya kujua hukumu ya kesi kati ya klabu yao na aliyekuwa mchezaji wa timu hiyo, Bernard Morrison ikiongezeka kila uchao, Kaimu Katibu wa klabu hiyo, Haji Mfikirwa, amewataka mashabiki kuwa na subira wakiisikilizia Mahakama ya Usuluhishi ya Kimichezo (CAS), kutoa uamuzi.

Tayari CAS imesikiliza kesi yao na iliahidi kutoa uamuzi hadi ifikapo Agosti 24, mwaka huu, tarehe ambayo imeshapita, jambo ambalo limezua sintofahamu miongoni mwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini juzi, Mfikirwa alisema na wao pia walikuwa wanasubiri majibu ya CAS, kuhusu kesi yao na sasa wanaendelea kuvumilia, lakini hawana budi kuiachia mamlaka husika kufanya kazi yake.

Alisema Wanayanga wanatakiwa kuwa na uvumilivu kusubiri mamlaka husika kutoa uamuzi wa kesi yao na wanatarajia kila mmoja kupata haki yake.

"Matarajio yetu ilikuwa ni kuona kwamba tunapata mrejesho wa kesi kwa kuwa haujatoka basi ni suala la kusubiri kwa kuwa kesi ina taratibu zake za majibu kutoka.

"Mashabiki na wanachama wasubiri na kuacha suala hili hadi hapo mamlaka husika itakapotoa taarifa hizo, kwa sababu hata viongozi tumekuwa makini kutaka kufahamu hukumu ya kesi hiyo," alisema Mfikirwa.

Alisema alikosa usingizi na kuwahi kufungua barua pepe ya klabu hiyo Jumanne, siku ambayo ndiyo ilikuwa tarehe ya kupata majibu kutoka CAS, lakini hakukuta taarifa yoyote kuhusu hukumu hiyo.

Yanga iliwasilisha kesi dhidi ya Morrison kupinga uamuzi wa Kamati ya Sheria, Maadili na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), ambayo iliamua kuwa Morrison ni mchezaji huru kutokana na sababu za kimkataba, ambaye baadaye alijiunga na Simba.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042


7 70856 541002 >